# *Alama Ya Mnyama Na Muhuri Wa Mungu 2*

Hebu na tuendelee tu kusimama kwa dakika moja tunapoinamisha vichwa vyetu kwa ajili ya maombi. Sijui, huku tumeinamisha vichwa vyetu, kama kunaweza kuwa na yeyote hapa ndani angetaka kukumbukwa katika maombi, acha tu ijulikane unapoinua mikono yako, na kusema, "Mungu, unirehemu, nina haja usiku wa leo, sana."

2 Baba yetu wa Mbinguni, tunakikaribia kiti Chako cha enzi, kiti Chako kikuu cha rehema, katika Jina la Bwana Yesu, Mwokozi wetu. Tunaiendea njia hiyo kwa sababu Yeye alitwambia tuje hivyo nasi tutapokea kile tunachoomba. Nasi tuna furaha sana kujua ya kwamba tunaweza kutulia mioyoni mwetu juu ya hakikisho hilo, kwamba yale usemayo, Wewe unaweza kuyatimiza. Kwa kuwa usiku wa leo tunajisikia ya kwamba sisi, kwa imani, ni Uzao wa Ibrahimu, na chochote kinyume na Neno la Mungu tunatenda kana kwamba hakikuwako, kwa sababu Mungu amesema kweli, nasi tunaamini Yeye anayo ile kweli, Naye ni Kweli.

3 Sasa, tunawaombea wale walioinua mikono yao, kila mkono, Bwana. Unajua kile walichohitaji, unajua kilichokuwa moyoni, wazo lenyewe la nia yao walipoinua mkono wao. Ninaomba ya kwamba utaziondolea mbali dhambi zao, uondolee mbali magonjwa yao, uwape shauku ya moyo wao, Bwana. Na waishi maisha marefu, yenye furaha hapa, ikiwezekana, wakuone kule Kuja kwa Bwana mara ya pili.

4 Tunaomba ya kwamba utalibariki Neno usiku wa leo, tunapofanya ushirika Kwalo, nikizungumza usiku wa leo juu ya hili jambo kuu mno papa hapa mlangoni petu, linaloendelea sasa katika miji yetu, na kote ulimwenguni. Tunaomba ya kwamba utatupatia Neno Lako, upako Wako, Bwana, tupate kujua tu jinsi ya kunena kama mausia ya Mungu. Tunaomba, katika Jina la Yesu. Amina.

5 Mwaweza kuketi. Ni jambo moja zuri sana na tukufu kuja katika nyumba ya Bwana. Nasi tumekuwa tukifurahia sana mkutano huu humu kanisani pamoja na Ndugu yetu Buntain na wahudumu wahusika katika—katika ushirika huu mkuu ambao tumekuwa nao, na watu wote, walei wote, na kutoka kwenye makanisa mbalimbali, kila kanuni ya imani, jamii, na aina.

6 Nilipokuwa nikishuka jukwaani usiku wa leo ilitokea tu kwamba nilikutana na baadhi ya marafiki zangu, nilikutana na Ndugu Allcock hapa, mara ya kwanza nilipomwona baada

ya miaka mingi. Ninakumbuka mara ya kwanza nilipokuwa Edmonton, Canada, ninaamini ulikuwa kule juu pamoja nasi wakati wa ule mkutano. Ndugu mmoja kutoka Uholanzi hapa, nafurahi kumwona, na watu mbalimbali njiani.

7 Nami najua kila mmoja wenu. . .ningetaka kuwa na wakati wa kuwapa mkono, na kwenda nyumbani na kuona jinsi. . . Ninajua mke wako ndiye mpishi bora kuliko wote nchini, ninajua tu hilo, kwa hiyo ninaliamini. Na kwa hiyo ningetaka kwenda nyumbani pamoja nanyi, lakini, ninaamini nilisema kitu kama hicho yapata miaka kumi na minne iliyopita huko Canada, lakini ni—ninatarajia kufanya hivyo moja ya siku hizi katika ule Utawala mkuu wa Miaka Elfu, ambapo tunaweza tu kuwa na wakati mwingi, haitubidi kuharakisha, watoto hawataumia, hakuna ninii, hakuna kitu kinachoweza kudhuru chochote.

8 Nami nilikuwa nikiwazia kuhusu kushuka, na—napenda milima, nami ninawazia juu ya wakati wa Utawala wa Miaka Elfu, ningependa tu kutumia miaka milioni chache nikizungukazunguka tu kote milimani, nikiangalia tu pande zote, na—napenda hilo.

9 Na—nafikiri kuhusu kukutana na dada fulani huko nje milimani, labda amekuwa huko kwa miaka milioni moja, akitembea, jinsi tu mama atakavyofanya, mwajua, pamoja na kama, akiwa na mbwa mdogo, ama chochote kile, lakini angekuwa akitembea pamoja na simbamarara mkubwa, ama chochote kile, ningesema, "U hali gani, Dada?"

Mbona, angesema, "Wewe ni Ndugu Branham."

"Naam."

"U hali gani? Hakika nimefurahi kukuona."

"Ungewazia muda gani sasa, kama ulikuwa ukihesabu wakati, ambao ungekuwa huku nje, kukiweko na kitu kama wakati."

10 "Loo, miaka milioni chache, hiyo tu, nilifanya matembezi kidogo." Loo, hilo si lingekuwa zuri sana? Na si namna fulani tu ya ndoto ya kubuni, ni ukweli, ni kweli, ni kweli kabisa. Tunaenda Mahali fulani, tuwe mtu fulani tutakapofika kule, na—napenda hilo.

11 Sasa, jana usiku tulikuwa katika Kitabu cha Ufunuo, na tukizungumza juu ya *Muhuri Wa Mungu Na Alama Ya Mnyama,* nami nikaziweka zote mbili pamoja. Jambo lingine, nilikuwa nimeandika Maandiko fulani, niliyaacha juu ya meza ya hotelini, ndipo Billy akayarudia, nami ni—nikatoka upesi, nilimsikia akipiga honi, akiniita. Na kwa hiyo niliwazia wakati alipokuwa ameshuka kwenda kuyachukua Maandiko yangu, ningependa kwa namna fulani kurudia kidogo kutoka jana usiku, na pia kufanya matangazo.

12 Sasa, nina jumbe tatu za kuhubiri kesho, kwa hiyo, nami. . . Moshi wenu kweli hausaidii sana koo langu, na, kwa kweli, linakuwa baya. Basi kesho asubuhi ninapaswa kuwa na matangazo kwenye Kiamshakinywa cha Wafanyabiashara wa Full Gospel kwenye Mkahawa wa Clifton, ninaamini uko kwenye Broadway, Mtaa wa Broadway, kuna miwili huko, huu wa 7 na Broadway, ambapo kiamshakinywa cha kawaida hufanyika. Nami na—nazungumza kwenye. . . kwenye matangazo, na mara baada ya matangazo, ni—ninataka kuzungumzia ku—kundi la waaminio pale; hiyo ni kesho asubuhi.

13 Halafu kesho usiku, hapa nyuma kwenye—kwenye maskani, ama kanisa, hasa. Ndipo, kesho usiku, nafikiri tunapaswa kuwa, tukifunga hapa kanisani, ingekuwa vema kama tungekuwa na mstari wa maombi kesho usiku. Mnaona hivyo? Baada ya—baada ya ujumbe, halafu tuwe na mstari wa maombi. Kwa hiyo nitawatuma wavulana huko kesho usiku saa kumi na mbili kamili, kusudi wasiingilie ibada iliyosalia, na kusambaza kadi za maombi, nasi tutaitisha mstari wa maombi kesho usiku na kumwombea kila mtu pale, sasa, kwa ajili ya uponyaji wa miili yao.

14 Halafu Jumapili alasiri, ni kwenye ukumbi wa manispaa, ukumbi mkuu, nafikiri ni mahali pakubwa mno. Nasi tunatumaini mnawaleta marafiki kadhaa pamoja nanyi, kwa sababu nafikiri unakaa yapata elfu nne mia tano, ama kitu kama hicho. Mara ya mwisho nilipokuwa kule, imekuwa kama miaka kumi na miwili, kumi na minne iliyopita, Ndugu Charles Fuller alikuwa na ibada kule wakati huo, Mkristo mashuhuri. Nina hakika ninyi nyote mnamjua Ndugu Fuller kutoka hapa nje. Na. . . [Ndugu fulani anasema, "Jumapili usiku."—Mh.] (Ati nini?) ["Jumapili usiku."] Jumapili usiku, naam. Jumapili usiku saa moja, nafikiri ndivyo, na halafu, hiyo ni Jumapili hii ijayo usiku, kufungwa kwa huu uamsho.

15 Kisha tunaenda kutoka huko hadi Vens-. . . [Ndugu mmoja anasema, "Visalia."—Mh.] Visalia. Loo, jamani, baadhi ya majina haya hapa! Wote mle ndani kila kitu ni ma-G, H na—na haya yote Mtakatifu, na Mtakatifu, na kama huu San *Jose* hapa juu, unasikika kwangu kama. Wananiambia ni. . .

16 Nilimsikia jamaa mmoja wakati mmoja akija kule, na (wakati nikimngojea Billy) akasema, akaingia, akasema, "Mama, unaweza kuniambia," alikuwa kwenye mkahawa, "Mtakatifu *Jose* ni wapi?"

Kasema, "Ati nini?"

Kasema, "San *Jose*."

"Hakuna mahali kama hapo."

Kasema, "Uko hapa, papa hapa kwenye ramani."

Kasema, "Hiyo ni San Jose."

Naye akasema, "Loo."

Kasema—kasema, "Kwani unatoka wapi?"

Akasema, "Kentucky."

Akasema, "Vema, huku nje," kasema, "J zote ni H."

"Vema," kasema, "Huko Kentucky tunaita *J*, *J* na *H*, *H*." Kasema, "Si—sijui jinsi mnavyofanya jambo hilo huku," akasema.

Akasema, "Naona uko kwenye huduma."

Akasema, "Naam, mama."

Akasema, "Utatoka lini hudumani?"

17 Akasema, "Loo, karibu *Huni* ama *Hulai*, mojawapo, nakisia." Akashika upesi sana, mnamo Juni au Julai, akasema, "*Huni* au *Hulai*." Kwa hiyo, majina haya yote ya Kihispania, ninayachanganya yote.

18 Kwa hiyo, lakini hii ni Ven-. . .popote ulipo, huko juu, ni mahali fulani kati ya Fresno na Bakersfield. Ndipo tukapata udhamini, kundi la wahudumu kule juu, nasi tuna siku tano usiku, kuanzia tarehe 22 hadi Jumapili. (Asante.) Nami nina siku tano usiku za ibada. Nasi tunaninii . . . Yeyote wa marafiki zenu huko juu, vema, tungefurahi wa—wakija kututembelea, tu—tutafurahia kuja kwao.

19 Sasa, ninii . . . tutakapoondoka, hatuwataki mwache tu kuja kanisani, sasa, tunawatakeni mwendelee tu kuja, endeleeni tu kuja, kwa vyovyote vile. Kama ningaliishi hapa, mimi, labda hili lingekuwa ndilo kanisa langu la nyumbani papa hapa, kama ningaliishi hapa, ningekuwa papa hapa. Ninalipenda, ni kanisa zuri sana, dogo, mnaye mchungaji mzuri hapa. Nami nina hakika ya kwamba mtu yeyote anayehubiri Injili Yote, ningewakilishwa hapo, kwa sababu hivyo ndivyo ninavyoamini. Sina neno dhidi ya yoyote ya hayo mengine, bali kwangu mimi tu, ladha ya—yangu, ushirika wangu ungekuwa huo.

20 Sasa, msisahau matangazo sasa, kesho asubuhi, Mkahawa wa Clifton. Ninyi mlio huko juu, ama mnaosikiliza, nadhani . . . Hivi ni matangazo ya moja kwa moja, ama hayo yanarekodiwa, ama hivi mnajua? Ni matangazo ya moja kwa moja, na kesho asubuhi. Wala sijui yanapitia kituo gani. Lakini basi nadhani ndugu hapa, hivi huna matangazo, pia, hapa, ndugu, Jumapili, ama ndivyo? La, hakuna matangazo. Na wahudumu wengine, tunathamini kundi hili zuri la wahudumu ambalo limekuwa likitusaidia, na, hapa katika mikutano, wengi wa watu wao wanakuja. Nami bila shaka na—nawathamini watu hawa. Ninataka kuwaambia jambo fulani hapa.

21 Nami ni—nilijaribu sana, na kumshawishi maskini rafiki yangu wa thamani asiupeleke huu kwenye ukumbi wa manispaa, nilimshawishi. Lakini aliwahurumia watu waliosema itawabidi

wasimame, na kadhalika. Lakini hii hapa sababu sikutaka jambo hilo, Ndugu. Sasa, ninajua ya kwamba wakati mwingine mnanisikia nikiyakemea madhehebu haya, bali hiyo si watu walio katika hayo madhehebu, hiyo—hiyo ni dhehebu lenyewe tu. Sasa, ninatambua jambo hili, ya kwamba kama tukishuka kwenda kule kesho usiku, ni . . . vipi kama . . .

22 Kama tungekuwa na ushirikiano kamili na wahudumu wote, ingekuwa vema kushuka kule chini, hiyo ni kweli, lakini, ama ninamaanisha Jumapili, samahani, kama mimi . . . tungalikuwa na ushirikiano kamili, wahudumu wote, ambapo wangeyafunga makanisa yao, na kadhalika. Lakini kushuka kwenda kule, baadhi ya watu walio wagonjwa watashuka kuja kuombewa, na labda wahudumu hawakujua hilo kabla ya wakati, kwa hiyo wana mipango yao wenyewe kwa ajili ya usiku huo. Nami si—sipendi kufanya hivyo, ndugu, mimi, hiyo ni kweli, si—sipendi kufanya hivyo, kwa sababu, hata hivyo, blanketi hii inaenea kote, pande zote mbili, mwajua. Hiyo ni kweli.

23 Nami ninaninii, kama kuna kitu ninachoheshimu, ni watu wa Mungu, watumishi wa Mungu. Na, wakati mwingine, kama . . . Unakuta watu wanaoshuku sana ulimwenguni, ni wahubiri, hiyo ni kweli, wao ndio wenye kushuku sana kuliko wote. Lakini na—nataka kusema ni kwa nini, kwa sababu wao ni wachungaji. Hiyo ni kweli. Wanawachunga kondoo wao, mnaona, wana haki ya kuwa na mashaka, na kungoja na kuchunguza. Lakini unapoona Neno na Mungu wakifanya kazi pamoja, huo ndio wakati wa kuingia pamoja nao, unaona, wakati, unapoona Neno na Mungu wakija pamoja.

24 Kwa hiyo nilitaka tu ndugu wahudumu wajue kwamba sababu ya huo kuwa huko chini ni kwa sababu ndugu huyo alifikiri kwamba labda ingewapa watu nafasi, wote, kuketi, moyo wake uko moja kwa moja juu yake, ninaona kile anachomaanisha, lakini kwangu mimi, nilitaka tu kukaa mumu humu kanisani papa hapa, na kuendelea. Lakini alisema Jumapili usiku kulikuwa na wengi sana waliorudishwa, na—na kisha kutangaza, pia, kwa ajili ya ibada za uponyaji, ingewafanya watu wengi zaidi waingie.

Kwa hiyo sasa, kesho usiku, ingieni saa kumi na mbili, nasi tutakuwa na m—mstari wa maombi kesho usiku, Bwana akipenda.

25 Kwangu mimi, jinsi ninavyojisikia kulihusu, tuna mstari wa maombi kila usiku, mnaona, kwa kuwa, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hakuna hata usiku mmoja, katika siku hizo tatu ama nne zilizopita usiku, ila ambao Roho Mtakatifu amekuja mkutanoni miongoni mwetu, akaenda miongoni mwa watu na kuwaita, akawaambia wao ni akina nani, wanakotoka, kile wafanyacho, na kadhalika, na shida iliyopo, na kitakachotukia, na yote namna hiyo.

26 Halafu watu, imani inainuka ndani ya watu, ninasema, "Sasa, ni wangapi hapa walio waaminio?" Mikono kote jengoni inainuliwa. "Sasa weka mikono yako juu ya mtu fulani, usijiombee mwenyewe, bali waombee, maana watakuwa wakikuombea." Mnaona?

27 Vema sasa, kama hilo si la Kimaandiko, silijui. "Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na mwombeane. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Mnaona? Hayo ni Maandiko. Kwa hiyo ninajisikia ya kwamba kila usiku, kila mtu anaombewa, na kuwekewa mikono, kila usiku, ninajisikia.

28 Sasa, mikono yangu isingekuwa zaidi ya mikono ya mtu mwingine yeyote, ni—ni mtu mwingine tu, bali mkono wa Mungu ndio unaotaka juu yako. Naye alifanya, Mungu Ndiye aliyetoa ahadi. "Ikiwa wewe. . . Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hivyo ndivyo tu Mungu alivyoahidi, kisha kutoka hapo, tunachukua kutoka papo hapo.

29 Sasa, tuyarudie Maandiko yetu na somo letu. Hivi, Ndugu Borders, ulisoma Maandiko? Vema. Ninapenda kusikia Biblia ikisomwa. Ufunuo, niliufungua moja kwa moja, mlango wa 7 ndipo tutakapozungumzia, zaidi sana, usiku wa leo, nadhani. Sasa, hebu turudie jana usiku kidogo tu.

30 Sasa, somo letu ni hili. . . Tulikuwa, kwanza tulikuwa na ibada za uponyaji, kisha tukaingia kwenye ibada za kuhubiri Injili, na sasa tuna siku mbili usiku za mafundisho, na kesho usiku na Jumapili usiku ni ibada za uponyaji.

31 Sasa, jana usiku tulianza kufundisha juu ya masomo hayo mawili, ambayo nilifikiri yalikuwa muhimu sana. Nami nisingesema lolote kuhusu haya isipokuwa nilifikiri yalikuwa yanahitajika. Mnaona? Jambo la kwanza ni kulionya Kanisa, hiyo ndiyo sababu mlinzi husimama kwenye mnara. Anapomwona adui akija, basi anawaonya wale walioko mjini. Ndipo basi mlinzi asipoonya, basi Mungu atahitaji damu ya huo mji mkononi mwake. Hiyo ni kweli. Lakini kama kweli akiwaonya, wala hao watu wasilitilie maanani, basi damu yao wenyewe iko juu yao.

32 Na hiyo ndiyo sababu ninaninii tu—ninaliweka tu jinsi lilivyoandikwa *Hapa*. Mnaona? Na halafu ni juu yako, na kwenye Siku ya Hukumu ninataka, nitakapoiaga dunia hii, kama ningali nina fahamu na ninaondoka, ninataka niwe ninaweza kusema, kama Paulo, "Hakuna damu ya mtu yeyote mikononi mwangu, kwa maana sikujiepusha na kuwahubiria habari ya kusudi lote la Mungu, kama nijuavyo mimi," jinsi tu lilivyo.

Asanteni kwa barua zenu za—za kutoa maoni na kadhalika, hakika ninazithamini sana.

33 Sasa, *Alama Ya Mnyama, Muhuri Wa Mungu*. Sasa, ni wangapi waliokuwa hapa jana usiku? Hebu tuone, walikuwa, wamekuwa darasani. Loo, karibu kila mtu, nadhani. Vema. Sasa, kwa hiyo kupata msingi mdogo ambao tunauendea usiku wa leo. Sasa, ilinibidi kuchukua masomo yote mawili na kuyaweka pamoja, kwa sababu yanaenda sambamba moja kwa lingine.

34 Nasi tunaona, nilitangaza kile nilichowazia yalikuwa hapo mwanzo, na sasa natumia Maandiko kuthibitisha ya kwamba nafikiri jambo hili ni kweli. Nafikiri ya kwamba Muhuri wa Mungu ni Roho Mtakatifu, Biblia inaunga hilo mkono, alama ya mnyama ni kumkataa Roho Mtakatifu. Kuna matabaka mawili tu ya watu, na upande wa wokovu na kukataa kulianza katika Mwanzo, kama vile kila kitu kingine kilivyoanza.

35 Aisee, nina muhtasari leo, uliosema, "Waweza kuthibitisha ya kwamba Assemblies of God ilianza katika—katika—katika Mwanzo?" Sijui kuhusu dhehebu, bali roho iliyo katika Assemblies of God ilianza katika Mwanzo, hiyo ni kweli kabisa. Pia makanisa mengine yote yaliyozaliwa mara ya pili yalianza katika Mwanzo, na yote *yanayodhaniwa kuwa* makanisa, makanisa ya kawaida tu, yalianzia katika Mwanzo. Na yote mawili yaliwakilishwa katika wale wana wawili wa kwanza, Kaini na Habili pia.

36 Kaini alipokea alama ya mnyama kisha akafukuzwa. Tunatambua ya kwamba yule nyoka, ambaye ndiye aliyekuwa amemdanganya mama ya—yake, alikuwa ni mnyama wala si mtambaazi, "Alikuwa mnyama mwerevu sana kuliko hayawani wote wa kondeni." Na Mwanzo 14, ama Mwanzo 4:15, hasa, ambapo Mungu alimtuma, alimtia Kaini alama, na mara Kaini alipotiwa alama, alitoka Mbele za Bwana. Mlilipata jana usiku sasa? Mlilisoma? Mara alama hiyo ilipokuja, alitoka Mbele za Bwana, akajitwalia mke katika nchi ya Nodi. Sasa, mnalipata? Mnaona jinsi hilo lilivyo? Kanisa. Sasa, Mungu . . .

37 Kaini alikuwa tu kama mtu wa kawaida. Alikuja, alikuwa tu kama Esau na Yakobo, tungeweza kufananisha hapo tena. Na kote katika Biblia tunaona roho hiyo ikipanda juu, ikija, ikija, na hatimaye inafikia upeo, papa hapa, katika wakati huu tunaoishi sasa, ninaamini.

38 Sasa, kama mtaangalia, Kaini alikuwa mwanadamu, mtu wa kawaida wa ulimwengu kama Esau, na—na alikuwa na mwelekeo wa kidini, kwa hiyo alijua kulikuwa na Mungu, aliamini hilo. Akapanda juu . . .

39 Sasa, mnaona, hapo ndipo ninapotofautiana na makanisa yaliyosema, "Jambo pekee unaloweza kufanya ni kuamini tu, naye Mungu anatambua hiyo kama haki." Vema, hiyo—hiyo ni kweli katika maana moja ya neno, ni sehemu ya kweli, bali si kweli yote.

40 Ndugu mzuri Mbaptisti alinijia si muda mrefu uliopita, kasema, "Ndugu Branham, Ibrahimu angeweza kufanya nini zaidi ya kuamini? Ibrahimu aliamini, ikahesabiwa kwake kuwa haki."

Nikasema, "Hiyo ni kweli, bali Mungu alimpa ishara, muhuri wa tohara kwamba alikuwa ametambua imani yake."

41 Sasa, Roho Mtakatifu ndiye Muhuri wa Mungu. Sasa, kama ukisema unaamini, wala hujampokea Roho Mtakatifu, basi Mungu hajawahi kuitambua imani yako bado. Hiyo ni kweli. Kwa sababu Muhuri ni kutambua kwamba Mungu amekamilisha na kuimaliza kazi Yake ndani yako, hiyo ni kweli, kwamba Yeye alitambua, hakika.

42 Mtu fulani alisema, "Kwa nini unaifanya rahisi hivyo, Ndugu Branham, ukisema, Yohana Mtakatifu 5:24?"

43 Huo ndio mwanzo wa hiyo Roho, hiyo ni kweli, ninaamini ya kwamba mtu, mara unapomwamini Bwana Yesu Kristo, ni sehemu ya Roho Mtakatifu. Unapotakaswa, sehemu nyingine ya Roho Mtakatifu inakusafisha, ndipo unajazwa na Roho Mtakatifu. Sawa. Sasa, "Bali yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele." Kuna aina Yake moja tu, hiyo ni Uzima wa Mungu.

44 Sasa, tunaona ya kwamba Kaini, alitengeneza madhabahu, na kuweka dhabihu juu yake, akashuka na kukiri imani yake katika Mungu, na kumwabudu Mungu. Kwa maneno mengine, kama tu vile mtu wa kidini siku hizi, karibu tisini na tisa kati ya mia moja, wanasema, "Hii *hapa*."

45 "Ndivyo vizuri sana ninavyoweza kufanya," Kaini alisema, "hii ni, ni—ni—nilijenga madhabahu, mimi ni mfuasi hapa kanisani, nilitoa dhabihu, hili ndilo bora zaidi ninaloweza kufanya, ichukue ama uiache, hiyo hapo."

46 Huo ni ninii tu, huo ndio msimamo wa watu siku hizi, "Ninaenda kanisani, ninawasaidia kufanya kila kitu. Tulijenga jengo zuri, tumefanya *haya* yote, na tumefanya *hayo* yote, na kila kitu. Nilichangia katika mfuko wa wajane, na ninafanya *haya* yote. Hayo hapo, mazuri kuliko yote ninayoweza kufanya, yachukue, ama uyaache."

47 Lakini Mungu atayaacha, aliyaacha pale kwa ajili ya Kaini, atayaacha hapo kwa ajili yako. "Iko njia ionekanayo kuwa sawa machoni pa mtu, lakini mwisho wake ni njia ya mauti." Kuna njia moja tu iliyoandaliwa kwa ajili ya Mungu, hiyo ni kupitia kwenye mkondo wa Damu hadi kwa Roho Mtakatifu. Bila hiyo, umekwisha, umekwisha, hutaingia kamwe.

48 Angalia, "Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kamwe kuingia katika ule Ufalme." Hiyo ni kweli. Huna budi kuja, haidhuru wewe ni wa kidini jinsi gani, yote ufanyayo, hayo hayana uhusiano wowote. Hayo yanakufanya raia mwema sana,

bali si raia wa Ufalme huo kule, labda wa ufalme huu hapa. Lakini Ufalme wa Mungu uko ndani yako, umezaliwa katika Ufalme. Ufalme huja katika. . . Ufalme wa Mungu ni Roho Mtakatifu, wewe ni wa Ufalme huo.

49 Hiyo ndiyo sababu wanawake hawakati nywele zao, hawavai kaptura; hiyo ndiyo sababu wanaume hawavuti sigara, na mambo kama hayo, wanatoka Juu, Roho wao huwafundisha haki, utakatifu. Hawa—hawaapi, hawa—hawatumii lugha mbaya, na kadhalika. Kwa nini? Wamezaliwa kutoka Juu, wao ni tofauti, wanatoka, raia kutoka Juu.

50 Na sasa, angalieni, lakini ulimwengu, wao wanasema, "Vema, mimi ni mfuasi wa kanisa. Mimi ni wa Assemblies. Mimi ni wa Foursquare. Hayo hapo, mazuri kuliko yote niwezayo kufanya, yachukue, ama uyaache."

51 Kama ungalichukua sahani ya supu na ilikuwa na buibui ndani yake, usingeinywa, ungeishtaki hiyo kampuni, iliyokupa hiyo. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, ungeishtaki. Usingeinywa hata iweje, bali unaachilia tu aina yoyote ya fundisho la sharti ishindiliwe shingoni mwako hadi nafsini mwako, hata hivyo, mwili huo utakufa, kwa vyovyote vile. Hiyo ni kweli.

52 Hapa wakati fulani uliopita, nilikuwa kwenye jumba la makumbusho, nao walikuwa na uchambuzi wa mtu aliyekuwa na uzito wa ratili hamsini, ratili mia moja na hamsini, hasa, mwili wake ulikuwa na thamani ya senti themanini na nne katika kemikali. Ulikuwa na karibu chokaa ya kutosha kunyunyizia kiota cha kuku, na *kiasi fulani* cha kalisi, na kila kitu, yote ikipimwa ilikuwa na thamani ya senti themanini na nne.

Kulikuwa na wavulana wawili wamesimama pale, mmoja akamwambia huyo mwingine, kasema, "John, sisi hatuna thamani kubwa sana, sivyo?"

Akasema, "Hiyo ni kweli, siamini tunayo." Ratili mia moja na hamsini, una thamani ya senti themanini na nne.

53 Sasa, wewe kwanza kabisa huna thamani nyingi, sivyo? Lakini hakika unaushughulikia huo wa senti themanini na nne. Utaweka koti la hariri la dola mia tano juu yake na kuinua pua yako juu, kama mvua ingenyesha, ingekuzamisha. Hakika unashughulikia huo wa senti themanini na nne. Naam, bwana.

54 Lakini una nafsi hapo ndani ambayo ina thamani ya dunia elfu kumi, halafu unamwacha ibilisi ashindilie chochote ndani yake, na kukiita haki na dini, badala ya kuchukua njia sahihi ya Mungu juu yake. Hiyo ni kweli. Nafsi yako ina thamani ya dunia elfu kumi, mwili wako una thamani ya senti themanini na nne tu, unaukokota huku na huku, hakika unaushughulikia, loo, unaunyoa, na kuutengeneza vizuri, lakini jamani, unauvika vilivyo, bali nafsi hiyo, hakika hutaivalisha hiyo, unaacha tu chochote kitakacho kijikokotee kwake.

55 Wakikupa huo wenye buibui, ungeushtaki huo m—mkahawa uliokupa, lakini kanisa linaweza kukwambia, "Peana mikono na mchungaji, useme unamwamini Mungu, abudu, na hilo tu ndilo unalopaswa kufanya." Kama hiyo ni kweli, basi Kaini alikuwa sahihi.

56 Lakini kumbuka, Mungu alimwambia Kaini, "Abudu kama ndugu yako, nawe utatenda vema." Lakini hakutaka kufanya hivyo.

57 Hivyo ndivyo ilivyo siku hizi, hawataki kumwabudu Mungu katika Roho na katika Kweli, wanataka tu kwenda kanisani na kuabudu jinsi kanisa linavyosema waabudu. Abudu jinsi Mungu alisema uabudu!

58 Yesu alisema, "Mungu ni Roho, nao wamwabuduo Yeye imewapasa kumwabudu katika Roho na katika Kweli." Hiyo ni kweli, ziweke pamoja, Neno na Roho pamoja. Na kama Roho yuko katika Neno, Neno litajidhihirisha Lenyewe. Hiyo ndiyo sababu hasa mnaona upambanuzi, na uponyaji, na mambo kama hayo, ni Neno lililodhihirishwa.

59 Yesu alisema, "Enendeni ulimwenguni kote mkahubiri Injili," Kamwe hakusema enendeni ulimwenguni kote mkajenge makanisa, ama mfanye *hivi na vile*, mambo hayo ni sawa, bali hakusema enendeni ulimwenguni kote *mkafundishe* Injili, Yeye alisema *mkahubiri* Injili. Kwa maneno mengine, kuhubiri Injili kungekuwa ni kuonyesha nguvu za Roho Mtakatifu (Paulo alisema, "Injili haikuja kwa Neno tu, bali kupitia nguvu, madhihirisho ya Roho Mtakatifu."), ingebidi iwe hivyo, neno lenyewe linalofuata lilisema, "na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Hiyo ni kweli. Hana budi kulidhihirisha Neno.

60 Na kama Roho yuko katika Neno, Roho wa kweli wa Mungu yuko katika Neno, "Mkikaa ndani Yangu, na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo, nanyi mtatendewa." Sawa. Mnaona? Linarudi tu moja kwa moja kwenye Maandiko. Huwezi kutoka kwenye Maandiko, yanajirudisha Yenyewe moja kwa moja na kujisawazisha Yenyewe kila wakati.

61 Lakini Kaini, alitaka kitu cha kupendeza. Sasa, jana usiku nilikuwa nikisema, kumbukeni, urembo, huo ndio mvuto wa jicho. Kanisa Katoliki lilijifunza hilo muda mrefu, mrefu sana uliopita, ya kwamba mlango wa nafsi ni kupitia kwenye jicho, kufanya urembo, na kadhalika, nao watu huvutiwa na hilo, Hollywood ilijifunza hilo muda mrefu uliopita, ibilisi alilijua hilo kabla yeyote wenu hajalijua. Hiyo ni kweli kabisa. Hizo ndizo mbinu alizotumia, jambo lile lile. Akajitengenezea ufalme mzuri zaidi. Daima umekuwa wa kupendeza.

62 Hata—hata ibilisi, baada ya ile laana kumjia, akawa nyoka, angali ni kiumbe kinachovutia. Angalieni jinsi anavyoweza kusogea kwa madaha, na jinsi rangi zake zinavyopendeza, hata laana yake haikuondoa urembo kutoka kwake. Je, ulifikiri

Yuda Iskariote alikuwa ni maskini mtu mlevi, mwenye ukosi ulioinuliwa juu, na nywele zilizochanwa upande? Uh-uh, alikuwa ni mjanja kweli, jamani. Naam, bwana, ibilisi ni mwerevu kupita kiasi kwa hilo.

63 Nilipoenda Pigalle, mimi na Ndugu Moore, nilipokuwa Ufaransa, tulifikiri tungewaona tu wale makahaba wa kale wa Pigalle, watu tu waliolemewa na dawa za kulevya, Shetani ni mwerevu sana kwa jambo hilo, ni wanawake warembo sana uliowahi kuwaona. Unaona? Yeye ni mwerevu. Dhambi inavutia, dhambi inapendeza, bali ni mauti. Hiyo ni kweli. Usiangalie urembo, angalia ukweli, sio urembo. Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, linaruka lipate urembo, nalo linakufa, hiyo ni kweli, maana linapata mauti. Sitaki kukaa sana juu ya hilo, ninaanza kuhubiri juu yake.

64 Lakini, hata hivyo, tunaona ya kwamba Kaini basi, alimwacha Mungu, naye akajitwalia mke kutoka kwenye kundi lingine, katika nchi ya Nodi. Hivyo ndivyo hasa mtu anavyofanya ambaye hatapanda aje akamwabudu Mungu katika Roho na Kweli, anaondoka na kujitwalia kanisa litakalomridhisha, anaondoka. Lakini kumbukeni, baada ya Sethi, alikuwa ni mfano, Habili, akiwa ndiye aliyeuawa, Sethi alipachukua mahali pake, ilikuwa ni ishara ya kifo, kuzikwa, na kufufuka kwa Bwana, kurudishwa tena. Angalia jinsi hizo mbegu zilivyoshuka, jana usiku.

65 Sasa, tuendelee hapa chini tupate baadhi ya Maandiko ye—yetu tuliyokuwa tukitumia. Muhuri ukiwa ndio alama, jinsi ambavyo muhuri ulitumiwa badala ya jina, unatiwa juu yake. [Ndugu Branham aliiga kutia muhuri—Mh.] Nalo Jina la Yesu Kristo ni Muhuri wa Mungu, haki ya Mungu. "Jina la Bwana ni Ngome imara, wenye haki huikimbilia wakawa salama." Huo ndio Muhuri wa Mungu? "Lolote mtakalomwomba Baba katika Jina Langu, hilo nitalifanya." Hiyo ni kweli? "Lolote mfanyalo kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika Jina la Yesu." Hiyo ni kweli? Kila kitu mfanyacho.

66 Naye Petro alisema kwenye Siku ya Pentekoste, "Tubuni, mkabatizwe kwa Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea Kipawa cha Roho Mtakatifu," Muhuri wa Mungu. Muhuri wa Mungu uliotiwa alama, utambulisho, ni Jina la Bwana Yesu. Naye Yesu anapoingia ndani yako, inamwingiza Roho Wake ndani. Haidhuru ungeandika majina mangapi upande wa nje, kama Roho yumo mle ndani, anaishuhudia Kweli.

67 Ndipo tunaona ya kwamba katika Edeni Mungu alimchukua na kumtia alama Kaini na kumfukuza, lakini Sethi alikaa Uweponi mwa Mungu, naye Mungu akampa mke wake. Hivyo ndivyo Kanisa la kweli, lilikaa Uweponi mwa Mungu.

68 Loo, laiti ningaliweza kumleta Paul Boyd, yule mwanahistoria hapa juu. Jambo lingine, alikuwa akingojea

kwa miaka mitatu apate mojawapo ya mahojiano ya kibinafsi. Wanasimama nyumbani, wanatoka Asia, kutoka Afrika, kutoka India, kutoka kila mahali, wanangojea mahojiano hayo kwa miaka mingi. Wanapoingia juu ya hilo, tunaketi hapo mpaka Roho Mtakatifu atakaponena. Na asubuhi ya leo tulipokuwa tukizungumza, maono yalitokea.

69 Hii ni ibada ya kiinjilisti, nyumbani kwangu na mahali mbalimbali, hapo ndipo unabii unapoendelea. Watu huja ambao hawajui waelekee wapi, nasi tunangojea papo hapo mpaka Roho Mtakatifu, hawasemi jambo moja, wanamwacha Roho Mtakatifu anene. Naye anaingia, na kulifunua, na kuwaambia yale wamefanya, yale hawana budi kufanya. Kuwa tu na mtu huyo mmoja peke yake. Na, loo, jinsi Mungu kiajabu!

70 Mkuu sana asubuhi ya leo, ilinibidi kutembea chini ya ukingo wa maji, kule chini, mahali fulani, nami nikakutana na mchungaji kule chini nilipokuwa nikijaribu, ilinishtua sana, nikijaribu kurudisha nguvu zangu tena kutoka kwa yale maono makuu, yenye nguvu yanayofunuliwa, na kufunua, na kusema, na, yale uliyofanya, yale ambayo hukupaswa kufanya, na yale ambayo huna budi kufanya, na yale yatakayotukia baada ya kuyafanya. Loo, huko ni kujua kwa Mungu. Na hakuna hata wakati mmoja, nitamwuliza mtu yeyote aliyepo, ama mahali popote, ambapo yaliwahi kusema lolote, pasipo kutukia kila wakati, vivyo hivyo hasa, kwa sababu Hilo haliwezi kusema uongo, ni Mungu, Mungu hawezi kusema uongo.

71 Loo, kuishi chini ya Roho Mtakatifu! Kumbukeni, Sethi alimpata mke wake, hapana shaka Mungu alimpa mke wake, alidumu na Mungu. Na sasa mwaminio atakayedumu na Biblia, na kudumu na Mungu, basi ataninii, Kanisa la kweli litakuwa Bibi-arusi wa Yesu Kristo. Huyo mwingine atakuwa na bibi-arusi wa ulimwengu, chochote tu, tuliona hilo jana usiku.

72 Na, pia, tunasoma hapo ambapo Kaini na Habili, ambapo wote wawili walianzia, na—na ndipo tukalileta Babeli, jinsi Babeli ilivyoonekana katika Mwanzo, na katikati ya Biblia, mwisho wa Biblia. Tulikuwa na mahali ambapo Yesu, wakati alipokuja jukwaani, na wakati alipoondoka jukwaani, Yuda alikuja vivyo hivyo; mpinga-Kristo na Roho Mtakatifu walikuja vivyo hivyo. Na Maandiko kwa ajili ya hayo katika Mathayo 27, kwa hiyo, 26.

73 Halafu tunaona hapa katika . . . Tunaona Israeli, tulichukua Israeli na kuwalinganisha na—na Moabu, jinsi ambavyo Israeli walidumu waaminifu, ule ukoo, wakweli. Nasi tunaona hapa ya kwamba Moabu, wa haramu, wa kimsingi kabisa, kama tu vile Israeli walivyokuwa, lakini Israeli, waliokuwa na ukoo wa kweli, walikuwa na ishara na maajabu yakiwafuata, walikuwa na nyoka wa shaba, uponyaji wa Kiungu, walikuwa na shangwe za Mfalme kambini, walikuwa na Mwamba uliopigwa kwa ajili

ya wokovu wao, walikuwa na Baba wa Mbinguni akiwalisha kutoka Juu, walikuwa na wakati mzuri sana, hawajafungwa nira na chochote, watu tu wasiofungwa na madhehebu wakielea kila mahali. Nao walikuwa wakiwadhihaki kwa sababu hata hawakuwa taifa, watu tu waliotawanyika.

74 Lakini, hili hapa, natumaini mnalipata, walikuwa wakielekea kwenye nchi ya uenyeji wao, mfano mkamilifu wa Kanisa la kweli siku hizi, wakielekea kwenye Nchi ya uenyeji wao. Amina. Wakizungukazunguka wamevaa ngozi za kondoo, na ngozi za mbuzi, na wahitaji, na kadhalika, bali tunautazamia Mji ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu. Hivyo ndivyo Kanisa la kweli linavyotembea siku hizi. Na wale wa kimsingi kama Moabu walivyokuwa, walitoka wakiwa na dhabihu kamilifu, kama Israeli walivyokuwa nayo, wa kimsingi tu, na kila kitu, kama vile Israeli walivyokuwa, bali hawakuwa na Roho.

75 Tunasonga na kwenda kwa Kaini. . .kwa Esau na Yakobo. Mungu alisema ya kwamba kujua tangu zamani, ya kwamba kuchaguliwa tangu zamani kwa Mungu huenda. . . Si kwamba Mungu alitaka kumhukumu Esau, bali akijua kile alichokuwa. . .Kama Mungu ni Mungu, Yeye alijua kila kitu. Alijua kila kiroboto aliyewahi kuwa duniani, alijua kila mbu angekuwa duniani kabla dunia haijaumbwa, alijua ni mara ngapi angeyapepesa macho yake na angetoa kiasi gani cha shahamu kama akitolewa. Yeye hana kikomo.

76 Ni nani anayeweza—ni nani anayeweza kusema kutokuwa na kikomo ni nini? Kama Yeye si asiye na kikomo, basi Yeye si Mungu, na kama Yeye alikuwa asiye na kikomo, Yeye alijua mambo yote tangu mwanzo. Na kwa hiyo basi Yeye angeweza kuchagua, si kwa sababu alitaka kuchagua, lakini kwa sababu kujua Kwake—Kwake tangu zamani kulimfanya ajue ni nani atakayekuwako, na ni nani asingekuwako. Hiyo ndiyo sababu Kanisa zima, kila mtu atakayewahi kuwa katika Unyakuo, jina lao liliandikwa katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, inasema Biblia. Hiyo ni kweli. Mungu alijua hilo.

77 Yesu alikuja kwa kujua kwa Mungu tangu zamani, *kujua* huko, naye Yesu alikuja kukomboa, ama kulinunua Kanisa hilo tena. Wahubiri ni kama kwenda kwenye kidimbwi na kutupa wavu ndani na kuuvuta. "Ufalme wa Mungu umefanana na mtu achukuaye jarife na kwenda ufukoni mwa bahari. Alipolivuta ndani alikuwa—alikuwa na buibui wa majini, nyoka, nyoka wakubwa, vyura, na chochote kile, bali alikuwa na samaki." Sasa, hatujui ni yupi aliye na ni yupi asiye samaki, jambo pekee tunalopaswa kufanya ni kuvuta juya.

78 Naye Ndugu Buntain amekuwa akivuta juya hapa kwa muda mrefu, nikatoka, nikachukua wavu wangu, nikavute juya

pamoja nawe, Ndugu Buntain. Ninautupa huko nje na kuuvuta ndani, hawa hapa wanakuja madhabahuni, wanasimama na kumkiri Kristo. Sijui ni yupi mbuzi, yupi ni kondoo, yupi ni buibui, ama chura, ama chochote kile, lakini Mungu alijua kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu ni nani alikuwa. "Wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Wala hakuna mtu awezaye kuja, asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Wote alionipa Baba," wakati uliopita, "alionipa, watakuja Kwangu." Hiyo ni kweli. Yeye alisema hivyo.

79 Sasa, sijui ni nani, ninatupa tu wavu, na kusema, "Njoni nyote, mliochoka na kulemewa na mizigo mizito." Basi Mungu anajua yupi ni yupi, sijui mimi, hakuna mtu mwingine anayejua, ni juu ya Mungu tu. Kwa hiyo ni—ni wajibu wetu kuendelea mpaka atakapokuja.

80 Sasa, basi lile Kanisa kuu likijiweka tayari. Nasi tunaona ya kwamba Esau na Yakobo, kabla hata mmoja wao kuzaliwa, Mungu alisema alimpenda mmoja, na akamchukia huyo mwingine. Basi kumbukeni, walikuwa mapacha, mama mmoja, baba mmoja. Mnalipata? Mapacha. Kila uamsho huzaa mapacha, bila shaka huzaa. Kuna mapacha waliozaliwa katika mtu wa kawaida na mtu wa kiroho. Ilikuwa ni huko nyuma katika bustani ya Edeni, Kaini na Habili, kitu kile kile, kilianzia huko, kinaendelea tu kushuka.

81 Basi angalia Kanisa, Yesu Mchungaji, Yuda mweka hazina, ndugu, kutoka kabila lile lile, na kadhalika, moja kwa moja katika kundi lile lile, kanisa lile lile, Mmoja Mchungaji, na huyo mwingine, mweka hazina, mmoja ibilisi, na Mmoja, Mungu. Hivyo ndivyo iendavyo. Yesu alisema, "Katika siku za mwisho hizo roho mbili zingefanana sana, ingewapoteza walio wateule kama yamkini." Amina. Kama yamkini, bali haiwezekani, nao wata—hawatafanya hivyo kamwe. Vema.

82 Lakini anapokea Muhuri wa kweli; na Muhuri wa Mungu ni Roho Mtakatifu. Sasa tuko chini kuanzia mahali tulipoishia jana usiku kwenye Ezekieli mlango wa 9. Ni wangapi walioisoma? Mlitoa furaha kuu? Isomeni, sasa. Hapo ndipo nabii alipotangulia kuiona Pentekoste, na kusema yatakayotukia, aliwaona watu sita wakija kutoka kwenye lango la juu, nao walikuwa na silaha za kufisha. Kumbukeni, mliona ilikusudiwa Yerusalemu pekee? Yerusalemu pekee, maana huko ndiko Wayahudi. . .Mungu huwashughulikia Mataifa kama watu binafsi, bali Israeli ni taifa, taifa la Mungu. Naam.

83 Mmishenari mmoja alisimama kanisani mwangu (Ninamsikia Ndugu Fred Sothmann mara moja moja, akisema, "Amina," huko ndani mahali fulani, yuko nje kwenye kusanyiko, kwa vyovyote vile, baadhi ya ndugu kutoka huko maskanini.), ndugu Myahudi, amekuwa akijaribu kuingia Israeli wakati wote, akijaribu kufanya jambo fulani kwa ajili ya Wayahudi,

kuninii. . .alisema alitaka kuwaleta kwa Bwana. Naye alikuja maskanini hivi majuzi asubuhi, naye akasimama wakati upako ulipokuwa ukiendelea, akasema, “Ndugu Branham, ningependa kukuuliza swali: Nitaingiaje Yerusalemu? Nimejaribu kila njia.”

84 Nikasema, “Nisingejua la kukwambia.” Yapata wakati huo Roho Mtakatifu akashuka, na kusema, “Sivyo, kwa sababu Israeli itazaliwa katika siku moja.” Daima, naam. Loo, tuko karibu. Loo, tutafikia hilo katika dakika chache sasa, Bwana akipenda.

85 Nasi tunaona ya kwamba kabla yale mauaji hayajaanza, sikilizeni sasa, msilikose, kabla hayo mauaji hayajatokea, alimwona Mtu akitokea, amevaa mavazi meupe. Nyeupe inawakilisha nini? Haki ya watakatifu. Sasa, naye alikuwa na ki—kidau cha wino cha mwandishi ubavuni Mwake, Yeye akapitia mjini, akaanzia Yerusalemu, na kuwatia muhuri wale waliougua na kulia kwa ajili ya machukizo yaliyofanywa katika mji huo. Hiyo ni kweli, enyi wasomaji wa Biblia? Ndipo wakati mauaji yalipoanza, Yeye alisema, “Usiwaachilie, wazee, vijana, watoto, watoto wachanga, chochote kile, angamiza kabisa kila mtu asiye na alama hii.” Mnaona? Hakuna kitu kilichosalia. Ama walipokea muhuri, au hawakuwa na muhuri.

86 Hiyo ndiyo sababu katika siku hii tunayoingia, tutalifikia moja kwa moja katika dakika moja hapa katika Agano Jipya, kwamba wataninii. . .Muhuri wa Mungu ni Roho Mtakatifu, na nje ya hapo ni maangamizi [Ndugu Branham anasafisha koo lake—Mh.] (Samahani.), kupotea.

87 Sasa, tumechukua maandishi ya Josephus jana usiku, na kadhalika, kama nilivyoyarejea, na wengi wa wanahistoria wengine wa kale. Josephus alitembea-. . .labda aliandika juu ya siku zile zile, na kuishi karibu na wakati Yesu wa Nazareti alipotembea duniani. Sasa, naye alinena habari zake, ya kwamba hao watu ambao, aliwataja, ninaamini, kama wala watu, waliokuwa wakila mwili wa Yesu wa Nazareti, bila shaka walikuwa wakila Ushirika, hakujua, yeye ni mtu tu ambaye hajaongoka, alikuwa tu ni mwanahistoria. Lakini yeye. . .

88 Waliondoka Yerusalemu kisiri walipoona jambo hilo likianza kutimia, kisha wakaondoka wakaenda Uyahudi, wakaondoka huko. Lakini Wayahudi, yale madhehebu makubwa yote yaliungana pamoja, kisha yakarudi, kasema, “Tutaingia katika nyumba ya Bwana. Yehova ndiye Kinga yetu, nasi tumeishi katika huu, Mungu aliijenga nyumba hii, Yehova alifanya *hili*, naye Sulemani akaliweka wakfu hekalu, hapa ni mahali patakatifu sana.”

89 Lakini walimkataa Masihi wakati alipowajia jinsi hasa unabii ulivyosema angekuja, na kufanya jambo lile lile ambalo Biblia ilisema angefanya, bali hakuja kulingana na theolojia yao. Natumaini hilo halitadhuru, bali natumaini litatia nanga

kwenye kilindi. Nao wakaja. Alionyesha ishara Yake ya Masihi jinsi hasa Biblia ilivyosema angefanya. Ni wangapi wanaoamini hilo? Hakika alionyesha.

90 Ishara ya Masihi ilikuwa ni gani? Alikuwa ni Mungu-Nabii. Mnaona? Halafu basi, na walipofanya hivyo, waliitaje ishara hiyo ya Masihi? Kuna mtu anaweza kuniambia? Waliiitaje? Beelzebuli, ibilisi, mpiga ramli. Kwa sababu aliweza kutambua mawazo yao, alijua walichokuwa wakiwazia, kuwaambia juu ya mambo haya.

91 Nao Wayahudi wa kweli, walisema ilikuwa ni nini? "Hiyo ndiyo ishara ya Masihi." Loo, Nathanaeli alisema, "Hakika, Wewe ni Mwana wa Mungu; kweli, Wewe ndiwe Mfalme wa Israeli."

92 Kasema, "Kwa sababu nilikwambia nilikuona kabla hujaja mkutanoni, basi u—unaamini? Uta—utaweza kuona mambo makuu kuliko haya basi." Unaona, lazima uamini *kwanza*, liamini, ndipo utaona mambo makuu zaidi.

93 Sasa, tunaona kilichotukia, lakini wa—wa—wanyofu, makanisa makubwa, madhehebu, Mafarisayo, Ma—Masadukayo, na Maherodia, na hao wote, walisema, "Yeye ni Beelzebuli." Iliwabidi kujibia jambo fulani, iliwabidi kuliambia kusanyiko lao, kwa hiyo wakasema, "Yeye ni wa ibilisi."

94 Sasa, kumbukeni hilo, nao walikuwa watu wa kidini, watu watakatifu, watu wacha Mungu, kadiri ulimwengu ulivyohusika, dhambi moja dhidi yao wangepigwa mawe. Wasomi, waliohitimu, wanafunzi wa seminari, katika mstari wa makasisi, nao walihukumiwa, naye Yesu alisema, "Ninyi ni wa baba yenu ibilisi." Basi usimhukumu Roho Mtakatifu wakati anapokuita hadharani kile ulicho. Unaona? "Kipofu akimwongoza kipofu, si wote wataanguka shimoni?" Bila shaka. Yaangalieni Maandiko, angalieni ile ahadi, mjue saa inayokaribia.

95 Hao wanafunzi waliojazwa na Roho Mtakatifu, waliotiwa alama hiyo kwenye vipaji vya nyuso zao, pale, Muhuri huo wa Mungu, wakaanza kuangalia, na walipoona yale Yesu aliyosema yakitimia, walitoka humo.

96 Na hebu nikwambie, afadhali utoke nje, pia, ndugu. Hmm! Ngojeni mpaka tutakapomaliza katika dakika chache, tuone jinsi tulivyo karibu. Loo, Yesu alisema jambo lilo hilo lingekuwa likitukia kabla tu ya kuja Kwake tena, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu." Aliahidi jambo hilo, akaliapia, Mungu aliliahidi, na kadhalika, kwa hiyo halina budi kuwa hapa.

97 Sasa ninataka kweli utoe tu koti la m—mvua kutoka moyoni mwako, ushushe mwavuli, weka tu mwavuli wako wa Kimethodisti pembeni, Baptisti yako huko pembeni, na Pentekoste yako pembeni, na hebu tuliangalie Neno la Mungu.

Mnaona? Yawekeni tu yote kule sasa, na hebu tuliangalie. Mnaona?

98 Biblia ilitabiri kwa nabii Ezekieli, naye Roho Mtakatifu akaja na kufanya kama tu alivyosema, na hata watoto wachanga, Biblia...wanahistoria walisema...Sasa kumbukeni, Biblia ilisema, "Msiache chochote, mdogo, wala kijana, wala mzee, wala wote." Wote ambao hawana Muhuri huu wa Mungu wangetiwa alama vinginevyo.

99 Basi angalieni ni nani aliyetiwa alama kutoka kwake? Watu ambao maishani mwote walitoa maisha yao kwa ajili ya makasisi, makuhani, na watu mashuhuri, makasisi wakuu, na wasomi. Sasa, ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Mbona, hakika ndivyo ilivyo. Hakika, ni kweli. Kama tu vile mso-... Watakatifu tu, watu wazuri tu, labda watu wema, raia wa—wa nchi, lakini huo si udhuru. Mungu anapotuma kitu fulani nawe unashindwa kutembea ndani yake, basi uko nje, hivyo tu. Ama ufanye, ama usifanye. Hivyo ndivyo ilivyokuwa.

100 Wote ambao hawakuingia ndani ya safina, walizama majini, wala hakuna lingine, haidhuru walikuwa ni akina nani. Hilo ni jambo lile lile, wote wasio katika Kristo leo hii wataangamia bila Kristo. Ni kweli. Kwa hiyo huwezi kusema, "Mimi ni Mmethodisti, ama Mbaptisti, ama Mpentekoste," ama chochote kingine, huna budi kuwa ni wa Kristo. Na kama wewe ni wa Kristo, unafanya kazi za Kristo, hiyo inashuhudia na kuthibitisha ya kwamba ndivyo ilivyo. Mimi...Hilo ni dhahiri tu kama Maandiko, ninajua jinsi ya kulisema. Hilo ni dhahiri tu kama pua kwenye uso huu mkubwa, ama pua kubwa kwenye uso wangu huu, hasa. Hiyo ni kweli.

101 Sasa, angalieni, jinsi alivyofanya jambo hilo. Sasa, walikuwa...Wale—wale walioonywa, waliondoka, nao hao wengine wote wakaingia mjini, naye mwanahistoria anasema, kwamba walikula nyasi zote kutoka mtini. Tito aliuzingira, huo mji, mji wa Yerusalemu, ulikuwa umeteuliwa. Sasa, wakati wetu umeteuliwa kwa ulimwengu wote, lakini huku kulikuwa ni kwa mji wa Yerusalemu kwa Wayahudi pekee.

102 Naye Tito, alipoingia, a—aliuzingira huo mji, akawaweka mle ndani miaka miwili au mitatu. Basi alipofanya hivyo, walikula nyasi kutoka mitini, magome kutoka kwenye miti, nyasi kutoka ardhini, na hata wakachemsha watoto wao kwa wao na kuwala. Mama waliwachemsha watoto wao wachanga na kuwala, wazimu, wenye kichaa. Ndipo hatimaye, alipobomoa akaingia, aliwachinja na kuwaua mpaka damu ikatiririka kwenye malango ya mji.

103 Mungu mkuu, Yeye aliyejaa upendo, Yeye amejaa upendo, kusudi awe upendo hana budi kufanya hukumu apate kuwa mwenye haki. Kwa hiyo Yeye ni Mungu mwenye rehema usiku wa leo, lakini, rafiki yangu, utakaposimama mbele Zake Hukumuni

kwenye Siku hiyo yenye giza, yenye mawingu, atakuwa ni Mungu aliyejaa hasira, Biblia ilisema hivyo, katika ghadhabu Yake.

104 Nilikuwa huko chini mbele, nami nilikuwa nikikata kutoka kwenye ninii yangu. . .nilikuwa na mkata mawe kule chini kutoka Colorado, alikuwa na jiwe fulani, naye alikuwa akikata, jiwe dogo nililotaka kumpelekea msichana wangu mdogo kitu kidogo cha kuwekwa shingoni mwake, msalaba mdogo. Na kwa hiyo, akasema, "Kata ninii. . .nionyeshe mahali pa kulikatia." Na lote lilikuwa safi, kisha likaonekana kana kwamba limeparuza, kama mawingu yakining'inia chini, nami nakaliweka hilo juu ya msalaba.

Ndipo huyo mama akasema, "Kwa nini ufanye hivyo? Kwa nini usikate ile sehemu nzuri, safi *hapa* nje?"

Nikasema, "Msalaba si mzuri, ni nembo ya mateso na aibu."

Akasema, "Vema, mbona hivyo?"

105 Nikasema, "Hayo ni mawingu ya ghadhabu ya Mungu. Mungu alimwaga ghadhabu Yake juu ya Kristo, Yule aliyepachukua mahali pangu pale Kalvari. Alikufa chini ya hukumu na ghadhabu ya Mungu. Mungu alimwaga hukumu Yake kali juu Yake, Naye akapachukua mahali pangu." Nikasema, "Nilikuwa mwenye dhambi, Naye akapachukua mahali pangu."

Ndipo nikaona machozi yakitoka machoni mwa huyo mwanamke.

106 Nikasema, "Sisi ni wenye dhambi, wala hatuna tumaini, bali Mungu alijua ya kwamba ilitubidi kuzistahimili hukumu hizi, naye Yesu akazichukua kwa ajili yetu. Na hayo mawingu yaliyotanda juu ya msalaba yalikuwa ni ghadhabu ya Mungu ikimwagika juu Yake. Naye aliichukua ghadhabu ya Mungu katika mwili Wake Mwenyewe tupate kuwa huru." Loo, ni hadithi ya jinsi gani! Ni kweli jinsi gani! Ghadhabu ya Mungu.

107 Sasa, sasa mnaona jinsi ilivyowakilishwa katika Ezekieli mlango wa 9 huko Yerusalemu. Sasa tunakuja kwenye Ufunuo. Na sasa ningewatakeni ninyi mlio na penseli zenu mwandike hili, ningewatakeni mwandike Ufunuo 14:6-12. Hao ni wale malaika watatu wa mwisho, malaika watatu. Baada ya wale malaika saba wa mwisho, kulikuwako na malaika watatu maalum waliotokea. Mliona hilo?

108 Na sasa nawatakeni mwaone hao malaika watatu wa mwisho: Malaika wa kwanza, hiyo ni Ufunuo 14:6-12, malaika wa kwanza alikuwa amepiga tarumbeta ya Injili, na kuihubiri Injili ya milele kwa ulimwengu wote; malaika wa pili kwa namna fulani alihubiri Injili ya utakatifu, mnaona, kwa sababu alisema ya kwamba kanisa lilikuwa limefanya uasherati; kisha malaika wa tatu akanguruma wapate kuitoroka alama ya mnyama.

109 Angalieni, malaika wa kwanza, kwenye yale matengenezo, Luther, alihubiri Injili; malaika wa pili, Wesley, utakaso, uasherati, alilinyosha kanisa; lakini Ujumbe wa tatu, Ujumbe wa Kipentekoste, unapaswa kuwa, yule mjumbe wa kweli, akiwaonya waitoroke alama ya mnyama, akisema, "Kila aipokeaye alama ya mnyama, huyo atainywea ghadhabu ya Mungu iliyomiminwa pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha ghadhabu, imwagwe juu ya watu."

110 Huo ndio Ujumbe wenyewe siku hizi, malaika wa tatu, Ujumbe wa tatu, Ujumbe wa mwisho. Ujumbe wa Kilutheri wa kuhesabiwa haki, Ujumbe wa Wesley wa utakaso, na Ujumbe wa Kipentekoste wa Muhuri wa Mungu, iepukeni alama ya mnyama, tokeni kwenye hizo kuta kubwa za Babeli, mtiwe muhuri katika Ufalme wa Mungu.

111 Angalieni, kifungu kinachofuata, cha 12. . .kifungu cha 13, "Heri wafu wafao katika Bwana." Ni nini kinachofuata? Har-Magedoni. Kanisa limeondoka basi baada ya huo Ujumbe wa malaika wa tatu. Tulikuwa tukihubiri hivi majuzi kanisani juu ya hao malaika, na kutoa wale malaika saba wa mwisho, na Ujumbe wa huyo malaika, ndipo upako huu maalum ukaja wa hizo nyakati tatu, hao malaika watatu wa mwisho.

112 Angalieni sasa, katika Ufunuo 7 Yohana alichukuliwa katika Roho akaingia Utukufuni, naye akaona jambo hili likija, akasema:

> . . .*Nikaona malaika wanne wamesimama katika pembe nne za nchi, wakizizuia pepo nne* (Sasa sikilizeni kwa makini, yawekeni Maandiko yenu tayari kuandikwa.) *wakizizuia pepo nne. . .upepo usivume* juu ya *nchi*. . .
>
> . . .hata walipokuwa *wamewatia muhuri watumwa wa Mungu wetu juu ya vipaji vya nyuso zao*.

113 Sasa, linganisha hilo na Ezekieli 9. Mnamwona akija na silaha za kufisha na kushikilia, mpaka yule mwandishi alipotokea na kutia muhuri.

Angalieni sasa, humu ndani:

> *Kisha nikaona malaika mwingine akipanda kutoka mashariki, mwenye muhuri ya Mungu aliye hai:*. . .

114 Akija kutoka mashariki, naye alikuwa awatie muhuri watumishi wa Mungu wetu katika vipaji vya nyuso zao. Sasa, tunajua ya kwamba Kanisa kamwe haliitwi watumishi, Kanisa ni wana na binti. Israeli ndio mtumishi wa Mungu, Ibrahimu alikuwa mtumishi Wake, Israeli ni mtumishi wa Mungu, bali Kanisa linaitwa wana Wake na binti Zake. Mliona? "Zizuie pepo nne." Muda gani? "Hata tutakapokwisha kuwatia muhuri watumishi," Israeli, "wa Mungu wetu katika vipaji vya nyuso zao."

115 Loo, hebu nirudi nyuma kwenye historia ndogo kabla hatujaendelea mbele zaidi. Angalieni kilichotukia, sasa, watumishi wa Mungu wetu, Israeli, Israeli walitawanyika, wakati mmoja wakaingia Babeli, ama, huko chini Babeli, ndipo waliporudishwa, hiyo ni mara ya pili, mara ya kwanza ilikuwa huko Misri, na halafu Babeli, kisha wakatawanywa na Himaya ya Kirumi.

116 Naye Yesu alisema katika Mathayo mlango wa 24, "Jifunzeni mfano. . . " Kama nilivyoanza kuwaonyesha jana usiku, walimwuliza maswali matatu, Naye akajibu maswali yao matatu. Lakini walipotaka kujua wakati wa kurudi Kwake ungekuwa lini, Yeye alisema, "Mwonapo mtini ukiisha kuchipusha, na miti mingine yote, jueni ya kwamba wakati umekaribia, hata mlangoni."

117 Sasa, maskini yule mnafiki anashika hilo, maskini mtu asiyeamini, na kusema, "Kizazi hicho kilipita, kizazi hicho kingine kimepita, Yeye alisema uwongo." Hakusema uwongo. Kwa sababu hawana matumizi ya kiroho ya Neno. Hakusema hicho kizazi wakati huo, Yeye alisema, "Kizazi kilichoona mtini ukichipusha majani yake."

118 Angalieni huko nyuma katika Yoeli, mlango wa pili, ambapo nilihubiri hapa si muda mrefu uliopita, wale wadudu wanne, "Yaliyosazwa na tunutu yameliwa na madumadu; na yaliyosazwa na madumadu, yameliwa na nzige." Mnakumbuka nikihubiri hayo? Nafikiri ilikuwa hapa California, kwenye kiamshakinywa, naamini ilikuwa ni Phoenix. Yaliyosazwa na Wamethodisti, yameliwa na Wabaptisti; yaliyosazwa na Wabaptisti, yameliwa na Wapentekoste, alikuwa ameuharibu huo mzabibu wote, "Lakini nitarudisha, asema Bwana, yote. . . "

119 Basi angalieni, mdudu yuyo huyo ni kitu kile kile, ila tu katika hatua mbalimbali. Tunutu anakuwa madumadu, na kadhalika, na kuendelea mbele, na huyo ni mdudu. Akaanza kula upendano wa ndugu, akichukua Biblia, na kuibadilisha na kitu kingine. Nami nikatoa mambo manne makuu na kuyathibitisha kwa Maandiko, vitu wanavyokula, mafundisho ya Neno la kweli la Mungu, upendano wa ndugu, kama Paulo alivyosema, tayari umeanza, katika Wakorintho wa Kwanza 13, mambo hayo yote, jinsi wanavyoyala, na kulila tu Kanisa moja kwa moja hata kwenye kisiki, bali Yeye alisema, "Nitarudisha, asema Bwana," hiyo ni kweli, "miaka yote waliyokula," na mambo yote waliyokuwa wamefanya.

120 Angalieni, Israeli, "Wakati ninyi," daima imekuwa ni huu mtini, "mtakapouona mti huu ukichipusha majani yake," kitu gani? Kile kizazi kitakachoiona Israeli ikifanyika taifa, kizazi hicho hakitapita mpaka yote yatakapotomia. Angalieni! Loo, hivi hamlioni? Hapa, waangalieni. Sasa, Mungu daima imembidi kuwafukuza Wayahudi, kamwe hawakuwa na Roho Mtakatifu.

Wengi wao hata wasingeamini manabii wao, wajumbe wao, na ilimbidi Yeye kuwafukuza.

121 Na hivyo ndivyo itakavyomlazimu kulifanyia kanisa la Mataifa, Itambidi kuvunja vizuizi hivi vya kimadhehebu. Tunauacha ukomunisti uanze kula karibu nasi, na ndipo itatubidi kuja pamoja. Mungu atalitimiza Neno Lake, kwa sababu lile agano halina masharti, si "Ukifanya, nitafanya," bali, "Tayari nimefanya hivyo." Hiyo ni kweli. Loo, ninapenda hilo! Hmm! Hilo linanifanya tu nijisikie kubarikiwa.

122 Angalieni kile alichofanya hapa sasa, si "Ukifanya, nitafanya," hilo—hilo liliisha wakati Adamu alipovunja agano lake, nayo Israeli ikavunja agano lake, tangu Kutoka 19, na kadhalika, bali hili ni, agano, ni neema. Mungu aliapa, akamwambia Ibrahimu, aliapa kwa nafsi Yake ya kwamba ingekuwa hivyo, naye akaapa kwa nafsi Yake. Kwa hiyo kupitia kwa Uzao wa kweli wa Ibrahimu ni Yesu Kristo, ambaye ni neema ya Mungu, wala hakuna sheria kwake tena, la, bwana. Sheria haina uhusiano nayo hata kidogo, uko juu ya sheria, juu ya sheria, ni upendo. Upendo uko juu ya sheria, neema. Torati ilikuja kupitia Musa, neema na kweli zikaja kupitia Yesu Kristo.

123 Laiti ningalikuwa na siku zingine zaidi usiku za kuhubiri juu ya *Msikieni Yeye* juu ya hilo, kwenye Mlima wa Kugeuka Sura, mngeliona kikamilifu, jinsi Mungu . . . tunachukua hilo na kulifanyia kazi mle ndani, na kuonyesha tu jinsi ambavyo hizo sheria, na walimu, na kadhalika, na kile kinachotukia.

124 Hata hivyo, sasa angalieni, Israeli, ilimbidi Mungu kuufanya mgumu moyo wa Farao kuwafukuza mara ya kwanza. Naye alifanya jambo lile lile wakati huu, akaufanya mgumu moyo wa Hitler dhidi ya Wayahudi, hilo ndilo lilioanzisha vita. Kumbukeni, Mungu alisema, "Yeyote alaaniye Israeli, nitawalaani, wale wawabarikio Israeli, nitawabariki." Nao ulitawanyika kote ulimwenguni. Ndipo akaufanya mgumu moyo wa Hitler, akaufanya mgumu moyo wa Mussolini, akaufanya mgumu moyo wa Stalin, mioyo yote mbalimbali ya taifa, Yeye aliifanya migumu, na hatimaye akafungua njia, nao Israeli wanarudi na tayari wako katika nchi ya uenyeji wao.

125 Ukitaka kuona ni siku gani ya mwezi, angalia kwenye kalenda, ukitaka kuona ni siku gani katika majira ya kuja kwa Bwana, angalia mahali Israeli wanapoketi, hiyo ndiyo saa ya Mungu. Huyo hapo, ameketi katika nchi ya uenyeji wake, bendera ya kale kuliko zote ulimwenguni, ile nyota yenye ncha sita ya Daudi, bendera ya kale kuliko zote ulimwenguni inapepea tena kwa mara ya kwanza kwa muda wa miaka elfu mbili mia tano. Naam, bwana. Naam, ile bendera iliyopaswa kuinuliwa juu. Israeli, Palestina ikichanua kama waridi, mlisoma kwenye magazeti, na mkaangalia jinsi walivyorudi, huko chini kabisa Irani, na kadhalika.

126 Gazeti la *Look* liliandika makala, jinsi walivyowatafuta hao Wayahudi. Wasingeingia kwenye ndege hiyo, maskini Rabi huyo alitoka akaenda kule, kasema, "Nabii wetu alitwambia, Isaya, mamia ya miaka iliyopita, maelfu ya miaka iliyopita, kwamba tutakaporudi kwenye nchi ya uenyeji wetu, tungerudi juu ya mbawa za tai. *Huyo* hapo ameketi." Amina. Wakapanda moja kwa moja wakaenda zao.

127 Wakati Ndugu Arganbright, mmoja wa ndugu zetu hapa, wakati, loo, wakati aliponileta huko kwenye Pwani ya Magharibi wakati huu, alikuwa huko akipiga picha. Picha zingine, ana moja ya *Dakika Tatu Kufikia Usiku Wa Manane*, nayo sayansi inasema hivyo ndivyo ilivyo, dakika tatu kufikia usiku wa manane. Nasi tunaangalia huko na kuona hao Wayahudi wote wamewekwa katika nchi ya uenyeji wao.

128 Lewi Pethrus, ni wangapi waliopata kusikia habari zake? Kanisa la Stockholm huko Uswidi, ndugu mzuri sana, aliniambia, "Ndugu Branham, Wayahudi daima wamewaamini manabii wao." Kasema, "Laiti ungalishuka kwenda Israeli!"

Nikasema, "Sawa, hilo linaonekana zuri kwangu."

129 Akasema, "Angalia, wao, niliwatumia milioni moja ya Agano hili, wanasoma kuanzia nyuma kwenda mbele, na—nao wanasoma Agano Jipya."

130 Waliwauliza Wayahudi hawa, wakasema, "Kwa nini mnakuja nyumbani, hivi mnawaleta baba na mama zenu, na hao vipofu, na wagonjwa, na kuwaleta humu, waje kwenye nchi ya uenyeji wapate kufa?"

Kasema, "Tumekuja kumwona Masihi." Amina.

131 Ndugu, usijali, Mmataifa, siku yako karibu imekwisha. Hebu niwaonye katika Jina la Bwana: Mlango wa Mataifa unafungwa hakika tu kama nilivyosimama hapa. Yesu alisema Waislamu pale wangezikanyaga kuta za Yerusalemu mpaka kipindi cha wakati wa Mataifa kitakapomalizika, ama kutimia. Huyo hapo, Israeli katika nchi ya uenyeji wao, taifa lenye jeshi lake lenyewe na pesa zake. Amina. Yeye ni taifa kamili sasa, mtini unachipusha majani yake, na tayari yamechipuka.

132 Basi walipofika kule, waliwapa hizi Agano Jipya, mwulizeni Lewi Pethrus. Walisoma Agano hili Jipya kuhusu vile Yesu alivyokuwa, kamwe hawakusikia habari Zake, walisema, "Kama huyu ndiye Masihi, basi hajafa, basi hebu tumwone akifanya ishara ya Masihi, nasi tutamwamini. Hebu tumwone akithibitishwa. Tunawaamini manabii wetu, naye Masihi atakuwa ni Nabii. Hebu tumwone akifanya ishara ya Masihi, Nabii, nasi tutamwamini kama Masihi." Loo, ni mpangilio mzuri jinsi gani, mkamilifu kabisa!

Nikasema, "Bwana, niruhusu niende."

133 Ndipo niliposhuka huko Cairo, Misri, kabla tu hatujakutana na Mfalme Farouk, nasi, huko Rumi, halafu tukashuka huko Cairo, Misri, nilikuwa nimeshika tiketi yangu ya kwenda mkononi, nikapanda juu, nao waliishaitangaza safari hiyo, ndipo Roho Mtakatifu akanena, na kusema, "Sio sasa, hii bado siyo ile saa, kuna kuokotwa zaidi kwa masazo."

134 Ilikuwa vigumu kwangu kuamini jambo hilo. Nikatoka nje nyuma ya hilo banda, Mungu ndiye Hakimu wangu, nami nikaomba, nikapiga magoti, nikasema, "Baba wa Mbinguni, saa moja tu ama mbili nami nitakuwa huko Palestina, nitawapa Wayahudi hao changamoto, na kusema, 'Je, mlisema kwamba kama Masihi huyo ndiye Masihi wa kweli, ati mwonyeshwe akifanya ishara ya nabii, nanyi mtamwamini?'" Ukimfanya Myahudi akuahidi, atatimiza neno lake. "Sasa, kama huyo ndiye Masihi wa Biblia, basi Yeye alikuwa ni Nabii, Naye angali ni Nabii. Sasa, kama akifanya ishara ya Masihi, mtamwamini?"

135 Moja kwa moja kwenye uwanja ule ule, niseme, "Jichagulieni kundi la watu, na mwaweke hapa nje, mahali fulani, mwone kama Yeye angali ni Nabii, ama si—ama siye. Acha waone ikitendeka. Ndipo moja kwa moja kwenye misingi ile ile ambapo baba zenu, babu zenu, walimkataa Roho Mtakatifu, Myahudi aliupeleka kwa Mmataifa, hapa Mmataifa akiurudisha kwa Myahudi."

136 Wakati Myahudi huyo atakapoipokea Injili, siku za Mataifa zimekwisha. Lakini Yeye asingeniruhusu niende. Kwa nini? Sijui. Hapa katika dakika moja tu, nasi tutawaonyesha katika Maandiko ni kwa nini.

137 Angalieni, aliifanya migumu mioyo yao. Sasa, ni lini kuliwahi kuwa na ugomvi kamili wa ulimwengu baada ya wakati huo? Ilikuwa ni Vita vya Kwanza vya Dunia. Majeshi yote, mataifa, yalikuwa yanakusanyika katika . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

138 . . . walikuwa wakiandika juu ya kufifia kwa Vita vya Kwanza vya Dunia. Hakuna mtu anayejua leo hii ni nani aliyeleta tangazo la amani. Kaiser Wilhelm alisema hakufanya hivyo, hakuna jemadari aliyesema hakulifanya. Lakini angalieni, jinsi ilivyokuwa ni ajabu! Ilikuwa tarehe 11 Novemba, saa tano [Kiingereza: Eleven o'clock—Mfa.] mchana. Siku ya kumi na moja ya mwezi, mwezi wa kumi na moja wa mwaka, saa ya kumi na moja ya siku, na dakika kumi na moja ifike saa tano [Kiingereza: Eleven—Mfa.]

139 Ilikuwa ni kitu gani? "Visimamisheni!" Vilisimama kiajabu. Ni kitu gani kilichosababisha hilo? Tangazo la Mungu lilitokea visimamishwe. "Zizuie pepo nne," (*Pepo* zinamaanisha, "vita na ugomvi," tunajua.) "mpaka tutakapowarudisha Israeli Palestina tena. Zizuieni hizo pepo nne."

140 Navyo vikakoma papo hapo kwenye saa ya kumi na moja, kwa sababu mnakumbuka Yesu akinena juu ya watu wa saa kumi na moja? Nao wale walioingia saa kumi na moja, Yeye alisema nini? Loo, msiwe bubu, iweni wa kiroho. Angalieni, Yeye alisemaje? Watu wa saa kumi na moja walipata ujira ule ule waliopata watu waliokuja saa moja. Basi ubatizo wa Roho Mtakatifu hauna budi kurudi moja kwa moja na kumtia muhuri Myahudi, kama vile yule wa kwanza alivyotiwa muhuri, hao watu wa saa kumi na moja. "Zizuieni hizo pepo nne, msiache ulimwengu uangamizwe mpaka tutakapowatia muhuri watumishi wa Mungu wetu kwenye vipaji vya nyuso zao."

141 Hiyo imekuwa karibu miaka hamsini iliyopita wakati Roho Mtakatifu amekuja kutoka mashariki, akawashukia watu, nao Wapentekoste, Mitaa ya Azusa, na kadhalika, wakaanza. Sasa, itakuwaje? Hawana budi kuzizuia, wasiiangamize dunia nzima, maana Yeye asingeweza kufanya hivyo wakati huo, kwa vyovyote vile, lakini sasa wana bomu la kawaida litakaloiangamiza dunia nzima. Hiyo ni kweli. Mzizuie mpaka kitu gani? "Hata tutakapokwisha kuwatia muhuri, katika vipaji vya nyuso, watumishi wa Mungu wetu." Loo, ndugu, haya basi, haya basi.

> . . .*kuwatia muhuri watumishi wa Mungu wetu katika vipaji vya nyuso zao*.

Naye anaendelea hapa, na kusema:

> . . .*nikasikia hesabu yao waliotiwa muhuri:*. . . walikuwa *watu mia na arobaini*. . .*nne elfu*. . .

142 Kawapa elfu kumi na mbili wa kila kabila. Loo, jamani, hivi hamwoni ninalomaanisha? Maandiko yakiliweka kikamilifu. Sasa, kumbukeni, wote wasio na huo, waliangamia.

143 Sasa, Vita vya Kwanza vya Dunia, Vita vya Pili vya Dunia, na sasa tuko tayari kwa Vita vya Tatu vya Dunia, vikijitayarisha kila mahali. Ni kitu gani? Israeli wako katika nchi ya uenyeji wao, wakimngojea Masihi wao. Kanisa la Mataifa, wakati wa Kipentekoste, Luther, Wesley, na sasa wakati wa Kipentekoste umekuwa vuguvugu, na kumtapika Yesu, Naye anawatapika, kweli, wakati wa Kipentekoste.

144 Lakini mwishoni kabisa kabla ya ulimwengu kuangamizwa, Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu," kwamba kanisa la Mataifa lingepokea nguvu zile zile, malaika yule yule, shahidi yule yule, ninii. . .Hakika, mnaweza kuona hilo, ni dhahiri tu iwezavyo kuwa, mtoto angeweza kuliona. Mnaona?

145 Haya basi, tuko kwenye wakati wa mwisho, kila kitu kinatangaza hilo. Popote unapotaka kwenda katika Biblia, iliyowekwa papa hapa, angalia hapa, ulimwengu una wasiwasi, kuna nini? Kila kitu, mataifa yanatetemeka.

Mataifa yanatetemeka, Israeli inaamka,
Ishara ambazo Biblia ilitabiri;
Siku za Mataifa zimehesabiwa, zimekumbwa na hofu kuu;
"Rudini, Enyi mliotawanyika, makwenu." (Hiyo ni kweli.)

Siku ya ukombozi imekaribia,
Mioyo ya watu inazimia kwa hofu; (Hiyo ni kweli, sivyo?)
Jazweni na Roho, taa zenu zimetengenezwa na ni safi,
Angalieni juu! Ukombozi wenu umekaribia.

Manabii wa uongo wanadanganya, Ukweli wa Mungu wanaukana,
Kwamba Yesu yule Kristo ndiye Mungu wetu.

146 Loo, ulimwengu huu una shida gani hata hivyo? Kuna shida gani? Loo, amkeni, enyi watu, mkamrudie Mungu! Mna shida gani? Hivi hamwezi kuona kule kutkiswa kukuu kwa Mungu, Malaika Wake akishuka, akitenda kazi, akifanya ishara zile zile na maajabu, yale hasa aliyosema angefanya, kila usiku, moja kwa moja mbele zenu?

147 Vema mwasema, "Inaonekana kana kwamba wanapaswa kujua huko Washington, DC." Yeye hakuenda kwa Kayafa, alikuja kwa walio Wake. Malaika huyu hakushuka kwenda Sodoma, hakuambatana na akina Billy Graham wengine wa kisasa, na hao wengine, walishuka kwenda kule na kujaribu kuwaita watoke, lakini Malaika huyu alikaa pamoja na Kanisa teule, Ibrahimu, aliyeitwa atoke. Amina. Whiu! Hmm! Utukufu! Ni ajabu jinsi gani!

148 Muhuri wa Mungu ni nini? Muhuri wa Mungu ni nini? Waefeso 4:30, "Msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mlitiwa muhuri hata Siku ile Kanisa litakapokombolewa liingie Utukufuni."

149 Sasa tena, mnataka kuweka Andiko lingine? Waefeso 1:13, Paulo akinena. Wagalatia 1:8 ilisema, "Kama Malaika kutoka Mbinguni, akija akahubiri jambo lingine lolote, na alaaniwe." Naam. "Mkiisha kuamini, mlitiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu wa ahadi. Mkiisha kuamini, nyinyi . . . "

150 Sasa, ndugu Mbaptisti, Mpresbiteri, hebu nikuulize jambo fulani: Ati unasema unampokea Roho Mtakatifu unapoamini? Paulo alisema, "*Mkiisha* kuamini, mlitiwa muhuri na Roho Mtakatifu," baadaye.

151 Matendo 19, Paulo alikutana na Wabaptisti fulani, Apolo, mwanasheria aliyeongoka, mmoja wa wanafunzi wa Yohana, huko juu wakihubiri Injili, wakiwa na furaha kuu, na kupaza sauti, na kumsifu Mungu, wangali hawakuwa na Roho Mtakatifu. Paulo alikuja kule, na kukaa usiku kucha pamoja

na Akila na Prisila, alikuwa gerezani kwa kuhubiri Injili na kumtoa msichana pepo. Ndipo akaja mahali walipokuwa, nao wakampeleka kwa—kwa, kwa sababu, walikuwa watengeneza hema, akakaa pamoja nao, ndipo wakaenda mahali Apolo alipokuwa akifanya mkutano huu. Baada ya ibada kwisha, Paulo akawaambia, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?"

Mtu fulani alisema hivi majuzi, "Sivyo ilivyo katika kile cha asili."

152 Ninakanusha hilo! Nenda kachukue *Tafsiri Asili*, uone kama haisemi jambo lile lile, "Je, mmempokea Roho Mtakatifu *tangu* mlipoamini?" Papa *hapa* ilisema, "Mkiisha kuamini, ndipo mlitiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu wa ahadi." Msimchukue bibi-arusi huyo vuguvugu huko nje, ingieni humu ndani, ingieni kwenye hadithi na mwipate. Panda kwenye huo mhimili pamoja na Kristo, Roho Mtakatifu, ukasikie kutoka Mbinguni.

"Je, mmempokea Roho Mtakatifu tangu mlipoamini?"

Kasema, "Hatujui kama, kama kuna Roho Mtakatifu."

Kasema, "Mlibatizwaje?"

Kasema, "Kwa Yohana, tumebatizwa."

153 Kasema, "Huo hautafanya kazi tena." Naye akaamuru wabatizwe tena kwa Jina la Yesu Kristo, akaweka mikono yake juu yao ndipo Roho Mtakatifu akaja juu yao, nao wakanena kwa lugha, na kutabiri, na kumtukuza Mungu, baada ya wao kuamini, kupaza sauti, na kuwa na wakati mzuri sana. Hawakuwa na Roho Mtakatifu bado. Loo!

154 Paulo alisema nini? "Kama Malaika kutoka Mbinguni akihubiri injili nyingine yoyote, na alaaniwe," kwa sababu Shetani anaweza kujigeuza. Lakini dumuni na Neno. Hiyo ni kweli.

155 Sasa, baada ya wewe kuamini, ndipo unakuwa Uzao wa Ibrahimu, Uzao wa kweli wa Ibrahimu wakati wewe... Tunakuwaje Uzao wa Ibrahimu? Tukiwa tumekufa katika Kristo, basi sisi ni Uzao wa Ibrahimu, na ni warithi pamoja na Ibrahimu kulingana na ahadi.

156 *Baada ya* iliyotajwa inamaanisha, "kazi iliyomalizika." Baada ya kuamini. *Baada ya* maana yake ni, "kitu ambacho tayari...kitu fulani kabla ya hapo," basi hii ni kazi iliyomalizika. Muhuri ni kazi iliyomalizika. Unapoandika barua yako kamilifu, vyovyote vile itakavyokuwa, unaitia muhuri kwa jina lako. Baada ya hiyo bahasha kukamilika kabisa, unaitia muhuri. [Ndugu Branham aliiga kupiga muhuri—Mh.] Unapotoka kwenda kwenye...

157 Nilikuwa nikifanya kazi kwenye barabara ya reli pamoja na baba yangu kwa muda, tulisaidia kupakia behewa. Niliangalia, tungelipakia huko nje. Tulipopakia behewa zima vizuri tu

lilivyoweza kuwa, behewa, mkaguzi alikuja, naye akalitikisa, akalikagua aone kama kuna kitu kilicholegea, kama kuna kitu kilicholegea, alilikataa.

158 Hiyo ndiyo shida ya Mkaguzi anayepita usiku wa leo. Yeye huyakagua maisha yetu sana, ndiyo sababu hatumpokei Roho Mtakatifu. Loo, huenda tukapiga mayowe, tukatenda kana kwamba tunaye, bali kwa matunda unajulikana, hivyo ndivyo unavyojulikana. Naye huyatikisa na kupata mahali padogo palipolegea *hapa* pa kutokuamini, mahali palipolegea kidogo *hapa*, mahali padogo palipolegea *hapa*, Yeye anayahukumu na kuyarudisha tena. Hayana budi kupakiwa vizuri, amina, maana una barabara ngumu ya kusafiria. Basi Mungu anapompa mwanamume ama mwanamke Roho Mtakatifu, Yeye hutikisa kila unyoya uliolegea ndani yao utoke, una safari inayokuja. Amina. Utukufu! Angalia kama amepakiwa vizuri.

159 Yeye alifanya nini? Kuhesabiwa haki, Yeye alimwita; utakaso, Yeye alimsafisha; Roho Mtakatifu, Yeye alimtia muhuri. Limepakiwa vizuri sana, basi wanafunga mlango. Basi jambo la mwisho ni lipi? Anatia muhuri kwenye behewa hilo la reli hadi kikomo chake, amina, sio hadi uamsho unaofuata, bali hadi kikomo chake. Amina. "Hivyo basi, msimhuzunishe Roho Mtakatifu wa Mungu, ambaye kwa yeye mmetiwa muhuri hata . . . "

"Uamsho unaofuata utakapokuja?"

La.

"Mpaka utakapowazia kujiunga na kanisa lingine?"

La. "Hata Siku ya ukombozi wako." Mungu anapokupa Roho Mtakatifu, ni kazi iliyomalizika. Amina.

160 Wakati mtoto mchanga, nilisema hivi majuzi usiku, anapozaliwa, kitu cha kwanza katika maisha ya kawaida ni nini? Maji huvuja, ni katika kuzaliwa kwa kawaida. Cha pili ni kipi? Damu inatoka. Kinachofuata ni kipi? Uhai unakuja.

161 Elementi zile zile zilizotoka kwa Kristo ndizo tunazopitia kuingia kwenye ninii Wake, kurudi katika Mwili Wake. Kitu cha kwanza kilichokuja kilikuwa nini? Wakamchoma ubavuni Mwake, maji yakatoka, Damu ikatoka, "Mikononi Mwako naiweka Roho Yangu."

162 Yohana wa Kwanza 5:7, kama ukitaka kuliandika, ilisema, "Wako watatu washuhudiao Mbinguni, Baba, Neno," ambalo ni Mwana, "na Roho Mtakatifu, hawa Watatu ni Mmoja. Lakini kuna watatu washuhudiao duniani, maji, Damu, na Roho, hao si mmoja, bali wanapatana kwa habari moja."

163 Huwezi kuwa na Baba pasipo kuwa na Mwana, huwezi kuwa na Mwana pasipo kuwa na Roho Mtakatifu, bali unaweza kuhesabiwa haki bila kutakaswa, unaweza kutakaswa bila kuwa na Roho Mtakatifu, lakini itakapomalizika, kuhesabiwa

haki na kutakaswa pia, Muhuri wa Bwana Yesu Kristo, kwa ubatizo, unawekwa juu yako. Amina. Nina dakika zingine kumi, natumaini haitubidi kuendelea na hili hadi kesho usiku. *Baada ya* inamaanisha, "kazi iliyomalizika imefanywa, tayari imekamilika."

164 Sasa, sasa, rafiki yangu wa thamani, sioni tofauti yoyote katika makanisa, yote ni sawa kwangu mimi, madhehebu. Na kama itanibidi kulitaja jina la kanisa hapa, silimaanishi kwa njia yoyote, kuna watu wengi wazuri katika kanisa hilo kadiri walivyo katika lolote lile, kwa sababu kuna Kanisa moja tu. Wala hatujaunganishwa ndani Yake, hatuna jina lolote katika Kanisa hili, ni Mwili tu wa Kristo, Mwili wa siri.

165 Mna madhehebu yenu basi, hilo ni sawa kabisa, maadamu huweki ua wako *hapa* chini, humruhusu ndugu yako aingie, unaona, ama kumhukumu. Jambo hilo, kama utatambua ya kwamba kuna ndugu *hapa*, na ndugu *hapa*, basi hilo ni sawa. Lakini watu, unapopata dhehebu, wanashikilia dhehebu badala ya msalaba na Kristo. Mnaona? Kwa hiyo wao . . .

166 Kama una dhehebu, nawe unaliandika, na kama ukimalizia kwa koma, "Tunaamini *haya* yote, pamoja na kadiri Bwana atakayotufunulia," hilo ni jema, lakini unapoimaliza kwa kituo kikuu, unakufa papo hapo. Basi nionyeshe moja ambalo halijamalizwa kwa kituo kikuu. Hakika, ndivyo ilivyo. Unaona?

167 Sio hao watu mle ndani, la, bwana. Kanisa Katoliki, kanisa la kwanza kujiundia dhehebu ulimwenguni lilikuwa ni kanisa Katoliki, mwulize mwanahistoria yeyote. Nionyeshe mahali palipowahi kuwa na dhehebu kabla ya hapo. Katoliki ni mama wa kila mmoja wao. Ufunuo 17 ilisema vivyo hivyo, ilisema yeye alikuwa ni kahaba, naye alikuwa ni mama wa makahaba. Sasa, wasingeweza kuwa ni wana, ilibidi wawe binti, hivyo madhehebu kahaba ya Kiprotestanti yako pamoja naye. Hiyo ni kweli. Tofauti yao ni nini? Yote mawili ni sawa. Mwanamke mchafu sana katika Long Beach anaweza kumzaa binti bikira, lakini kama akichukua tabia za mama yake, anakuwa kile mama yake alicho. Hayo ndiyo yale hasa yaliyoyapata hasa makanisa yetu ya Kiprotestanti.

168 Nitaelekeza usikivu kwa kanisa moja la kimadhehebu, kanisa la kwanza lililopata kunena nami juu ya Yesu Kristo nilipokuwa mwenye dhambi, ni la Waadventista wa Siku ya Saba. Mwadventista wa Siku ya Saba alisema Muhuri wa Mungu ndiyo sabato Yake, kwa sababu muhuri unaonyesha kazi iliyomalizika, kwamba Yeye ametiwa muhuri katika Sabato. Na kuadhimisha siku ya Sabato ni kumbukumbu ya kwamba umetiwa muhuri.

169 Sasa, ninyi Waadventista mnajua jambo hilo, mnamjua Dk. Smith, na lile Shirika la Kusomea Biblia Nyumbani na hayo yote. Ninayo yote kwenye chumba changu cha kusomea, na

Mashahidi wa Yehova wote na kadhalika namna hiyo, kufikia mahali popote wanapoinuka, ninajua hoja zao, mnaona, ninajua wanakoelekea. Kwa hiyo sasa, siku ya Sabato si muhuri, siku ya Sabato ilikuwa ni muhuri wa uumbaji wa Mungu, Yeye aliumaliza wakati huo na kuutia muhuri, hiyo ni kweli, kwa Sabato Yake, bali ilikuwa ni mfano wa Sabato ya Kikristo.

170 Sasa, baada ya Yeye kumaliza uumbaji Wake, Yeye aliwapa Sabato kama muhuri, hiyo ni kweli kabisa, kwamba alikuwa amemaliza uumbaji Wake. Ndipo alipomaliza mpango Wake wa wokovu, alikuwa na Muhuri mwingine.

171 Sasa, ndugu yangu Mwadventista, ninataka kukuuliza jambo fulani. Hiyo ni kweli kabisa. Sabato, hilo kwa namna fulani ni neno geni. *Sabato*, kwa kweli, ni neno la Kiebrania ambalo linamaanisha "p-u-m-z-i-k-o, pumziko." Ni siku ya kupumzika, siku ya Sabato, unaacha kufanya kazi na kadhalika. Mungu alimaliza kazi Yake, hakurudi tena.

172 Waebrania 4 inazungumzia jambo hilo hapo, "Yeye. . .Kwa maana Mungu alistarehe siku ya Sabato. Naye alisema katika mahali fulani, wakati mwingine, katika Daudi, leo, baada ya muda mrefu sana, ukiisikia Sauti Yake, usiufanye mgumu moyo wako. Basi kama Yesu angaliwapa Sabato nyingine, Yeye angalinena habari zake baadaye. Bali imesalia kuadhimisha Sabato kwa watu wa Mungu, kwa kuwa sisi tulioingia katika raha Yake, tumestarehe katika kazi zetu kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi Zake."

173 Ni wakati gani tunapoingia katika raha Yake? Sasa, ninyi mlio na penseli zenu, fungueni pamoja nami Isaya 28:8-12. Hapa ndipo unapoipata:

> *. . .amri juu ya amri;. . .kanuni juu ya kanuni; huku kidogo, na huku kidogo*. (Shikilia sana yaliyo mema.)
>
> *Bali kwa midomo ya watu wageni, na* kwa lugha nyingine *nitasema na watu hawa;*
>
> Na *hii ndiyo* Sabato, *hii ndiyo* raha niliyosema itakuja: Na kwa haya yote *wasingesikia*, wanaondoka wakitikisa vichwa vyao, na kadhalika.

174 Alisema ya kwamba muhuri wa kumalizia wokovu, Luther, kuhesabiwa haki; Wesley, utakaso, lakini Sabato itakapokuja, siku halisi ya raha, ingekuwa ni wakati "midomo ya watu wageni na lugha nyingine nitasema na watu hawa," na hii ndiyo kazi iliyomalizika. Haleluya! Huu ndio Muhuri, hii ndiyo Sabato.

175 Hivi hamwoni? Ni Roho Mtakatifu, ndugu. Hapo ndipo unapoingia katika kazi iliyomalizika. Kama ndio kwanza uhesabiwe haki, hilo ni sawa, hilo ni zuri; kama umetakaswa, hilo ni jema, bali unapompokea Roho Mtakatifu, ni kazi iliyomalizika, naye Mungu amekamilisha mpango Wake wa wokovu, na kuutia muhuri kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu.

Amina. Loo, jamani! Ni wangapi wanaoamini hilo? Roho Mtakatifu kila mahali katika Biblia ni kazi iliyomalizika, na Mungu alimaliza kazi Yake.

176 Aliwaita wanafunzi Wake kwa kuhesabiwa haki, akawatakasa katika Yohana 17:17, akawapa nguvu dhidi ya pepo wachafu, walitoka na kutoa pepo, kisha wakarudi wakishangilia, Yeye alisema, “Msifurahi kwa sababu mnatoa pepo, nao wanawatii, bali furahini kwa kuwa jina lenu limeandikwa Mbinguni.”

177 Ninataka kukuuliza jambo fulani sasa, ndugu yangu: Kama jina lako limeandikwa Mbinguni, hilo bado linatosha? La, bwana. La hasha. Yuda alikuwa papo hapo nao. Yuda alikuwa ni bata mkubwa tu kwenye kidimbwi kama hao wengine walivyokuwa. Alikuja moja kwa moja kupitia kuhesabiwa haki, akapitia utakaso, akawaombea wagonjwa, akawa na matokeo makuu, lakini ilipofikia Pentekoste, alionyesha rangi zake.

178 Na hivyo ndivyo hasa makanisa ya kimadhehebu yamefanya leo, wamepitia katika kuhesabiwa haki, kutakaswa, lakini inapofikia ubatizo wa Roho Mtakatifu, lundo la lugha, na ishara na maajabu, na—na Malaika wakitokea, na kadhalika, hawataki uhusiano wowote nalo. Kwa hiyo basi zimefanana sana hata ingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Utukufu!

179 Mtaniita mtakatifu anayejibingirisha kwa vyovyote vile, nadhani ndivyo nilivyo. Sijawahi kujibingirisha bado, lakini kama Yeye angeniambia kamwe, ningeshuka moja kwa moja kupitia *pale*, nikijibingirisha kwa nguvu niwezavyo. Afadhali nijibingirishe, kuliko kutoingia kabisa, kwa hiyo, sawa kabisa.

180 Angalia, ndugu, ni kweli. Kumbuka, Yesu alipokuja, Danieli, alimjia yule Mzee wa siku, Mzee wa siku, ambaye nywele Zake zilikuwa nyeupe kama sufu, ambalo linamaanisha Yeye alikuwa Hakimu, kama vile mahakimu wote huvaa wigi ya sufu nyeupe, mahakimu.

181 Mnaona Yeye alikuwa amejifunga mshipi katika Ufunuo matitini, si kama kuhani *hapa* chini kiunoni, juu ya matiti, namna *hii*, kama hakimu, joho la hakimu, unaamua. Hiyo ndiyo sababu Yohana hakumwona kwenye siku yoyote ya Sabato, ama Jumapili yoyote, alimwona katika Siku ya Bwana, kule kuja kwa Bwana wakati alipokuwa Hakimu, si, si siku hizi zingine.

182 Tunamwona humu ndani sasa, tunamwona wakati alipokuja, Danieli alimwona, na Yeye alikuja na kumi elfu mara kumi elfu ya watakatifu Wake. Hiyo ni kweli? Ndipo vitabu vikafunguliwa, na Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho kilikuwa ni Kitabu cha Uzima, na kila mtu. . .Mnaona? Hilo hapo kanisa lako vuguvugu linakuja, bikira aliyelala, Huyu hapa yule wa kweli pamoja Naye akitoka Utukufuni, baada ya kuwa kwenye Karamu ya Arusi. Na kulikuwako na mwenye

dhambi. Kiti Cheupe cha Enzi kilikuwa, Hukumu ikawekwa, Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi. Loo, haya basi.

183 Hapa kanisa hili linakuja moja kwa moja, Yuda alifanya kazi moja kwa moja hapo, alikuwa akidanganya kwa kuhesabiwa haki, akaingia katika utakaso, akatoka akaenda akawaponya wagonjwa, na kufanya ibada za uponyaji na kadhalika, kisha akageuka, lakini ilipofikia kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, alionyesha rangi yake.

184 Sasa, rafiki yangu wa Wesley, Mnazarayo wangu, Mpilgrim Holiness, sio kuumiza hisia zako, usiliite kundi hilo la watu wanaonena kwa lugha wendawazimu, usiwaite kundi la watakatifu wanaojibingirisha, na—na kupiga mayowe namna hiyo, kwa sababu papo hapo Yudasi anakuja moja kwa moja.

Nawe unasema, "Utakaso wote ndio Roho Mtakatifu."

185 Natofautiana nawe, utakaso ndio unaosafisha hiyo bilauri Roho Mtakatifu ndiye anayeijaza bilauri. Hiyo ni kweli kabisa. Sawa.

186 Hii *hapa* bi—bilauri. Vipi kama nikiipata *huko* nje? Imejaa matope, huko nje kwenye kitalu cha kuku, mahali fulani. Je, wewe mwanamke ungeweza kwenda na kumtilia mume wako maji kidogo katika hiyo? Vema, nisingetaka kuwa mume wako, lakini, basi kama ukifanya hivyo. Jambo la kwanza unalofanya ni nini? Unaiokota kutoka kwenye udongo wa matope, huko ni kuhesabiwa haki. Ndipo unafanya nini? Unaichukua na kuiweka katika mchakato wa kuchemsha, na kuua vijidudu, na kuisafisha.

187 *Kutakasa* kunamaanisha nini? Ni neno ambatani la Kiyunani ambalo linamaanisha, "kusafishwa na kuwekwa kando kwa ajili ya utumishi." Hiyo ni kweli. Neno *takasa* katika Kiingereza linamaanisha, "fanya safi," katika Kiebrania linamaanisha, "fanya takatifu." Na—na katika Ki—Kiyunani, linamaanisha "kutakasa." *Kutakasa*, *kusafisha*, na *takatifu* ni kitu kile kile. Ni nini? Imetakaswa, na kutengwa kwa ajili ya utumishi.

188 "Lakini heri ninyi mlio na njaa na kiu ya haki hii, kwa maana mtajazwa," kutumikishwa na kutiwa muhuri, "hata Siku ya ukombozi wenu." Loo, ni Muhuri wa Roho Mtakatifu, ndugu, huo ndio Muhuri wa Mungu. Hiyo ni kweli, kutiwa muhuri.

189 Sasa, Wayahudi ndio wa pili kuupokea. Wapentekoste wamekuwa nao, Wamethodisti, Wabaptisti, wote wanaotoka kwenye madhehebu mbalimbali wameketi papa hapa usiku wa leo. Mimi mwenyewe ni Mbaptisti, ama nilikuwa, ningali ni Mbaptisti, bali mimi ni Mbaptisti-Mpentekoste aliye na Roho Mtakatifu. Mimi ni Mnazarayo-Mpentekoste-Mpresbiteri-Mbaptisti. Loo, mnajua ninalomaanisha, yote katika hayo. Jambo ni kwamba, ni Roho Mtakatifu, ndiye aliyeleta tofauti, ndiye ambaye alinitia muhuri katika Ufalme wa Mungu.

190 Huyo ndiye aliyemtia muhuri kila Mmethodisti, kila Mkatoliki, kila Mpresbiteri. Sisi sote ni wanadamu, na kwa Roho mmoja, sisi sote hatujaunganishwa katika kanisa moja, sisi sote kuingizwa ndani kwa kupeana mkono mmoja, maji mamoja, bali kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa kuwa Mwili mmoja kwa Roho Mtakatifu, na kutiwa muhuri hata Siku ya ukombozi wetu. Amina. Huyo ndiye Roho Mtakatifu.

191 Sasa, mnaamini? Sasa, kumbukeni, duniani kutakuwa tu na matabaka mawili ya watu. Ninachelewa sasa, sina budi kufunga tu. Mnaamini? Ni wangapi wanaoamini ya kwamba Roho Mtakatifu ndiye Muhuri wa Mungu? Sasa, kumbukeni, tulionyesha mema na mabaya moja kwa moja, kanisa hili lingine vuguvugu, ndugu tu wa kimadhehebu (Mnaona ninalomaanisha?) akipitia kando.

192 Kama tu vile inavyosema pale, wengi wanachanganyikiwa katika hiyo Waebrania hapo. Mnaona? "Kama tukifanya dhambi makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi." Mchukue mama, kama . . .

193 Mtu fulani aliniuliza, "Hilo linamaanisha nini? 'Kama tukifanya dhambi makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi.'"

194 Vema, bado hajaingia ndani yake. Hiyo ni kweli. Alipokea tu ujuzi wake.

195 Ni kama tu katika Israeli, wakati Israeli walipoanza kuvuka wakienda kwenye nchi ya ahadi, waliwatuma wapelelezi, wawili wao wakarudi, kasema, "Tunaweza kuiteka," Yoshua na Kalebu.

196 Huyo mwingine akasema, "La, hatuwezi." Kwa hiyo walirandaranda papo hapo mpakani mpaka wakafa, nao walioamini ahadi wakaingia.

197 Kama vile mwanamke . . . Mvulana anapata wito maishani mwake, akasema, "Vema, Mama alifua nguo kwenye ubao wa kufulia apate kunipeleka shuleni, ninataka kuwa mhudumu."

198 Vema, naye anakuwa mhudumu. Anaondoka na kupata Ph.D. yake, ama digrii ya udaktari, ama chochote a—anachopata, kisha anarudi, Shahada yake ya Sanaa, ama chochote kile, anarudi, kwa vyovyote vile yeye ni mhudumu. Ndipo daima ana tamaa mbaya, na kadhalika, kanisani mwake, akina mama, na mambo mbalimbali, labda yeye huvuta sigara, na anajua hapaswi kufanya hivyo. Kasema, "Mungu, hilo halionekani zuri kwa mtu wa Mungu, basi niondolee kitu hicho." Yeye ametakaswa.

199 Anakuja moja kwa moja mpakani tena, anaangalia papo hapo upande wa pili na kuona ubatizo wa Roho Mtakatifu, bali anasema, "Nikifanya hivyo, madhehebu yatanitupa nje." Rudi, ukafie kwenye nchi ya mpakani basi ukitaka.

200 "Yeye atendaye dhambi. . ." *Dhambi* ni nini? "Kutokuamini." Ninataka mtu fulani aniambie tafsiri moja ya dhambi mbali na *kutokuamini*. "Yeye asiyeamini amekwisha kuhukumiwa." Hiyo ni kweli. "Yeye ambaye. . . " Hata hupati ninii ya kwanza. . . Vipi kama. . . ?

201 Kufanya uzinzi si dhambi, kuvuta sigara, na kunywa pombe si dhambi, hizo ni sifa za kutokuamini. Kama ungekuwa ni mwaminio usingefanya hivyo. Unaona? Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli kabisa. Mnaona, hiyo hapo, kutokuamini. Ni kitu gani? "Kama tukikosa kuamini makusudi," huyo ni wewe hapa nje usiku wa leo Mpresbiteri, Mmethodisti, ama wewe usiye na Roho Mtakatifu. "Kama tukikosa kuamini makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."

202 Unampa Mungu kisogo, unafanya nini basi? Unajitia muhuri nje, na kuchukua alama ya mnyama, kisha unaondoka kama Kaini alivyofanya, kutoka Mbele za Mungu. Hilo linatetemesha, sivyo. Unakuja moja kwa moja mpakani, halafu huamini, unaamini, bali unaogopa kulichukua.

203 "Yeye atendaye dhambi makusudi," asiyeamini makusudi, "baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli . . . " Linukuu hilo pamoja nami: "Yeye atendaye dhambi makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi. Bali kuitazamia hukumu yenye kutisha."

Na—na, "Mimi nitalipa, asema Bwana." Na, "Ni jambo la kutisha kuanguka katika mikono ya Mungu aliye hai."

204 Baada ya kuletwa moja kwa moja kwako na kukuonyesha ya kwamba huo ndio Muhuri wa Mungu, na kwa sababu tu ya sifa, ingekubidi kuacha kitu fulani, ama kuacha dhehebu lako, ama—ama kitu fulani upate kuupokea, kisha uuondokee, unajua unachofanya? Unajitia muhuri nje ya Ufalme, alama ya mnyama.

205 Wakati Mungu alipomwambia Habili, au, alipomwambia Kaini, kasema, "Nenda tu kule ukaabudu kama ndugu yako, umlete mwana-kondoo, ushuke uje hapa, uabudu kama ndugu yako," kasema, "utafanya vema. Fanya kama ndugu yako afanyavyo, utakuwa sawa."

Lakini asingefanya hivyo, kasema, "Hii ndiyo bora zaidi niwezayo kutoa, unaweza kuichukua au uiache." Basi akatiwa alama, ndipo akatoka Uweponi mwa Mungu.

206 Sasa, hili linaweza kuumiza, lakini, ndugu, nitakapofika kule kwenye ile asubuhi kuu, yenye dhoruba, moto ukishuka kila mahali, na watu wakipiga mayowe na kulia, nami nasikia maskini ile Mashua okozi ikipiga honi, ninataka kuwa na hakika kwamba tiketi yangu ni sawa, ndugu. Kama vile yule mzee mweusi alivyosema, "Bwana, ni—ni—nililizungumza Nawe muda mrefu uliopita, sitaki shida yoyote mtoni." Hiyo ni kweli. Sitaki shida yoyote mtoni, la, bwana. Afadhali ulirekebishe sasa.

207 Sasa, baada ya usiku huu liko mikononi mwako. "Yeye atakayekataa kuamini makusudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli," akamwona malaika wa Bwana akija, akithibitisha kila kitu katika siku ya mwisho, akiona Injili ya milele ikihubiriwa na Luther, akiona utakaso ukihubiriwa na John Wesley, na sasa Injili hapa ndani ikiwaonya dhidi ya kutiwa alama, "Usiondoke, mkaribie Kristo."

Unasema, "Sasa, Ndugu Branham, ati hiyo ndiyo alama?"

208 Naam. Hebu niwape Andiko dogo hapa kwa dakika moja tu. Ninawatakeni mfungue pamoja nami katika Kutoka, ama si lazima, liandikeni tu, Kutoka 21:6. Kama mtumwa alikuwa ameuzwa, kisha uje mwaka wa yubile. . .

209 Mwaka wa yubile, kuhani wa yubile alipiga baragumu. Ni wangapi wanaojua hilo? Baragumu ilikuwa ndiyo baragumu, naye akaipiga, na alipofanya hivyo, kila mtumwa angeweza kuwa huru, kurudi nyumbani kwake.

210 Kama alikuwa huko nje shambani akilima kwa jembe, na mtu hapa akimcharaza kwa mjeledi, naye akasikia, "Hiyo ilikuwa ni nini? Hiyo ilikuwa ni nini?"

Baragumu ya Injili ikilia, habari njema.

211 Atupe jembe hilo chini na kugeuka moja kwa moja, aseme, "Huna mamlaka juu yangu tena. Ninaenda nyumbani kwa mke wangu na watoto. Niliuzwa hapa utumwani, lakini hivi umeisikia hiyo baragumu ikilia? Hiyo inamaanisha kwamba mimi ni Mwebrania, nina haki, mimi ni mtu mwenye haki ya mzaliwa wa kwanza, nina haki, ninaweza kuwa huru bila pesa za mtu yeyote."

212 Sio "Kama utafanya *hivi*, ama ufanye *vile*." Mnaona kitu hicho chote kilikuwa ni neema. Amina. Sio "Ukipenda," bali, "Kama utasikia baragumu, mwaka wa yubile." Bwana alihubiri mwaka uliokubalika, Mwaka wa Yubile. Jinsi tungeweza (lakini ninaangalia saa hiyo) kuendelea katika hiyo.

213 Lakini kama ukiisikia baragumu! Unaona, *kusikia*. Imani chanzo chake ni kitu gani? Kusikia. Sasa, si—sio tu kusikia kwa sikio lako, bali kama *ukisikia* hilo linamaanisha unalielewa, unalikubali. "Ninakusikia, ninaamini." Mnaona? Ni kusikia.

214 Stefano alisema, "Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa moyo wala masikio!" Mnaona, wasiotahiriwa, wangeweza kulisikia kwa masikio bali wasiotahiriwa, wasingeweza kuamini hilo. Mnaona? "Wasiotahiriwa moyoni wala masikioni," kulielewa.

"Loo, yote ni siri kwangu," (Kama vile Kaini, "Ichukue ama uiache.") "Nilijiunga na kanisa, hilo ndilo zuri niwezalo kufanya."

215 Vema, ewe Kaini, utatiwa alama ya mnyama, kisha uingie moja kwa moja katika dhehebu lako. Ndugu, unaweza kumjia

Kristo na kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu. Unaweza kujichagulia.

Sasa angalieni, mnasikia ninii ya Injili . . . Baragumu ya Injili ni nini? Habari njema, Roho Mtakatifu yupo hapa.

"Unajuaje Yupo?"

Mwangalie akifanya kazi, angalia yale afanyayo. Ndiyo habari njema.

Sasa, vipi kama mtu huyu angesema, akikatakata, kasema, "Vema, siamini ninataka kwenda."

216 Uh-loo, kuikataa, walifanya nini? Walimchukua, ilimbidi bwana wake kumpeleka kwenye kanisa la Methodisti, Baptisti, Pentekoste, ama Presbiteri, na kumpeleka uku—ukutani, na kuliegemeza sikio lake ukutani, na kuchukua uma na kutoboa tundu kwenye sikio lake na kumtia alama. Wala kamwe hakuwa huru tena.

217 Basi kama ukiisikia kweli na kuiacha, basi sikio lako limezibwa wala hutaisikia tena. Utaondoka Uweponi mwa Mungu, ukisema, "Mama yangu alikuwa Mpresbiteri, mimi ni mzuri tu kama hao wengine."

218 Mama yako aliishi katika Nuru yote aliyokuwa nayo, bali huyo si wewe. Hiyo ni kweli. Kayafa aliishi katika Nuru yote aliyoijua, bali Yesu alikuwa duniani wakati huo. Hao waumini wote wa Kiothodoksi, wao—wao walikuwa na mashirika yao makuu, madhehebu, na kila kitu, walitembea katika Nuru yote waliyokuwa nayo, bali ile Nuru ilikuwa moja kwa moja mbele yao, bali walikuwa na shingo ngumu, wasiotahiriwa moyoni wala masikioni, hawakutaka kufanya hivyo. Ndipo Mungu akawafungia ndani kwa muhuri. Waliwaangamiza moja kwa moja huko Yerusalemu, kisha wakafa, wakaenda kuzimuni. Hiyo ni kweli.

219 Fanya chaguo lako. Mwamini Bwana Yesu Kristo, na ujazwe na Roho Mtakatifu. "Jazweni na Roho Wake, taa zenu zitengenezwe na ziwe safi."

Itakuwa Nuru wakati wa jioni.

220 Hiyo ni kweli. Wakati Nuru za jioni zinaangaza, kwa nini usizipokee? Kwa nini usije Kwake? Usifungiwe nje na muhuri, usiketi umekufa, mwamini Bwana Yesu Kristo, na utiwe muhuri katika Ufalme.

221 Alama ya mnyama ni nini? Kumkataa Roho Mtakatifu, mnaona, mkwamia mpakani, mnaona, akisha kuufikia ujuzi wa ile kweli. "Kwa maana haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru," mnaona, wakiufikia ujuzi wa ile kweli, na kuona kwamba wanaiona ile kweli, na kuona ujuzi wake, na kuona iko hapa, kuiona ikifanya kazi, kuona ni sahihi, na kuwa na ujuzi wa ile kweli, kisha kugeuka tena, "haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi."

222 Kama tu vile Kaini hapo mwanzo, ndivyo itakavyokuwa kwenye mwisho, hiyo ni Waebrania mlango wa 10, na atatiwa alama mbali na Uwepo wa Mungu na awe Mbaptisti, Mpresbiteri, ama Mpentekoste kwa dhehebu pekee, siku zao zilizosalia zote. Watalitumikia dhehebu badala ya kumtumikia Kristo, watumikie kanuni zao za imani, uwe Mkatoliki, uwe Mmethodisti, uwe Mprotestanti, ama chochote kile. Lakini kama wewe. . .si. . .Kama wewe ni wa Kristo umetiwa muhuri na Roho Mtakatifu, wewe sio, utatiwa alama moja ya siku hizi, na ninii tu, utashughulikia dhehebu lako, hayo ndiyo yote utakayopata kujua, kisha uhukumiwe mwishowe.

223 Baba yetu wa Mbinguni, saa zinaingia giza, wakati umekaribia, "Mataifa yanavunjika, Israeli inaamka, kila ishara ambayo Biblia ilitabiri," inatimia. Uliahidi mambo haya yote, Nawe ukasema yangetukia, tunajua ya kwamba ni kweli. Ninaomba, Baba, ya kwamba Wewe utakuwa mwenye rehema leo, na utawaokoa waliopotea. Tujalie. Na jalia watiwe muhuri kwa Roho Mtakatifu wala wasimkatae Mwokozi. Tujalie, katika Jina la Yesu. Amina.

Loo, jamani! Ninajua nimesema kweli, najua. "Kondoo Wangu wataisikia Sauti Yangu," Yesu alisema, kama alivyosema pale. Ishara. . .

"Unajuaje Yeye yupo hapa?"

224 Sikilizeni, Roho Mtakatifu yuko papa hapa sasa, ninamsikia akinena kwa lugha, anafasiri, ninamwona akifanya ishara na maajabu. Na kumwona hata. . .Nayo ishara ya mwisho ilikuwa iwe ni ishara ya Masihi. Yesu alisema, "Ninii tu. . . "

225 Ni ishara gani ya mwisho aliyokuwa nayo Ibrahimu kabla tu ya Sodoma kuteketezwa? Malaika huyo alisimama pale, Mungu Mwenyewe katika mwili. Tumechukua hilo, sivyo? Ibrahimu alimwita, *Elohimu*, Mungu. Alisimama pale Mgeni, na angalieni vile alivyomwita Ibrahimu, akamwita Ibrahimu kwa jina lake jipya, alilipata tu siku chache hapo kabla, badala ya *Abramu* alikuwa ni *Ibrahimu*. Akamwita Sara jina lake la binti mfalme, "Ibrahimu, yuko wapi Sara, mkeo?" Alijuaje alikuwa ameoa, na alijuaje alikuwa na mke, na alijuaje jina lake lilikuwa Sara?

Kasema, "Yuko hemani nyuma Yako."

226 Kasema, "Nitaninii," *Mimi*, kiwakilishi nafsi pale, "nitakuzuru kwa muhula wako. Unajua nitafanya jambo hili, nilikuahidi. Umeingojea kwa miaka ishirini na mitano."

Naye Sara, moyoni mwake, akacheka, na kusema, "Nitapata furaha pamoja na Bwana wangu, kwa kuwa mimi ni mzee na nimepita miaka ya kuzaa? Yeye ni mzee, pia."

Ndipo yule Malaika akasema, "Kwa nini Sara akacheka, akisema moyoni mwake, 'Haiwezekani kabisa'?"

227 Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu.”

228 Yeye ali—aliyahukumuje mataifa?

Wakati aliposimama na Petro, na kusema, “Jina lako ni Simoni, wewe ni mwana wa Yona.”

Akasema, “Loo, hilo ni, hilo ndilo!”

Wakati Filipo alipokuja, akamwona Nathanaeli, akamwambia Nathanaeli, kasema, “Hakuna kitu kizuri kingeweza kutoka—kutoka Nazareti.”

Kasema, “Njoo, uone.”

Naye alipokuja, akamtazama, alisema, “Tazama Mwisraeli kwelikweli, ambaye hamna hila ndani yake!”

Kasema, “Rabi, ulinijua lini?”

Kasema, “Kabla Filipo hajakuita, ulipokuwa chini ya mti, nilikuona.”

229 Akapitia njia ya Samaria. Hao walikuwa ni Wayahudi, sasa ni—sasa ni Wasamaria. Si Mataifa, hatukuwa tukimtazamia Masihi yeyote, tulikuwa na rungu mgongoni mwetu, tulikuwa makafiri, mnaona, tukiabudu sanamu, kwa hiyo Yeye hakufanya hivyo mbele ya Mataifa. Lakini kama alifanya hivyo kwa Wayahudi na Wasamaria . . . Kuna jamii tatu tu, watu wa Hamu, Shemu na Yafethi. Sasa, kama Yeye alimfanyia hivyo yule mwanamke Msamaria . . . Alikuwa amemwendea, Yeye akasema, “Nipe maji ninywe.”

Akasema, “Aha, si kawaida Kwako, ukiwa Myahudi, kumwomba mwanamke Msamaria kitu kama hicho.”

Naye akasema, “Lakini kama ungalijua ni Nani unayesema naye!” Kasema, “Nenda, kamwite mumeo basi.”

Akasema, “Sina mume.”

Kasema, “Hiyo ni kweli, ulikuwa na watano.”

230 Akasema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa, tunajua, tu—tuna waalimu wazuri huko chini nchini mwetu, hapa chini Samaria, tunajua ya kwamba Masihi ajapo, Yeye atafanya jambo hili, lakini u Nani Wewe?”

Akasema, “Mimi Ndiye.”

Akaingia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu Ambaye ameniambia mambo niliyofanya. Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi?”

231 Nayo Biblia ilisema walimwamini Yeye kuwa ni Masihi kwa sababu ya yale aliyomwambia yule mwanamke. Alijua zaidi juu ya Mungu kuliko nusu ya wahubiri wa Hollywood, kweli, hiyo ni kweli, akiwa katika hali yake, kwa sababu alifunzwa na Roho Mtakatifu. Haya basi. Yeye ni Mungu, Yeye angali ni Mungu, bila shaka Ndiye.

232 Mwangalieni mtini asubuhi hiyo alipoangalia chini, Zakayo alikuwa anaenda kujificha, aone mahali alipokuwa. Alipopitia pale, Yeye, vema, alisimama, na kusema, "Zakayo, shuka, ninaenda nyumbani pamoja nawe kwa chakula cha jioni."

233 Mwangalieni kipofu Bartimayo akimgusa huko nje, "Ewe Mwana wa Daudi, uturehemu!" Akamsimamisha Yesu, na shamrashamra hizo zote zikiendelea. Mnaona, Yeye alijua hilo.

234 Mwangalieni yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, akakimbia na kuketi chini. Mnaona? Akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

235 Petro akamkemea, kasema, "Kwa nini kusema jambo kama hilo? Waangalie watu hapa, wakikupa mikono, na kukuita *Rabi*, ama kadhalika. Kwa nini ukasema jambo kama hilo?"

236 Kasema, "Lakini nimekuwa dhaifu, nguvu, nguvu zilinitoka." Akaangalia kote, akamwona maskini mwanamke aliyefanya hivyo, akasema, "Imani yako imekuokoa, kutokwa kwako na damu kumekwisha."

237 Sasa, Yeye aliahidi jambo lilo hilo kwenye kumalizia kwa wakati wa Mataifa. Ni wangapi wanaoamini hilo? Aliahidi jambo hilo katika Biblia. Sasa, je, Yeye hutimiza ahadi Zake? Hiyo ni kweli. Ninakupa changamoto uamini. Amina. Hivyo ndivyo ninavyojua Yeye yupo hapa. Mnaamini? Iweni tu na imani, wala msilititilie shaka, liaminini. Biblia ilisema, "Kama unaweza kuamini." Hiyo ni kweli? Mwaminini Bwana Yesu Kristo.

238 Mwanamke huyo aliyeketi papo hapo anamwombea binti yake, anatokwa na damu kwa ndani. Unaamini kwa moyo wako wote? Vema, unaweza kupata kile unachoomba basi. Amina.

Simjui mtu huyo, sijawahi kuwaona maishani mwangu. Unaamini kwa moyo wako wote?

239 Moja kwa moja huko nyuma, huko nyuma kabisa, hivi hamwoni Nuru hiyo inayosimama papo hapo? Iko juu ya mwanamke mweusi aliyeketi kwenye safu hii ya mwisho, huko nyuma. Amevaa nguo ya samawati yenye ukosi mwekundu, kidogo ni nyeupe. Anamwombea shemeji yake aliye na kansa. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Simama huko nyuma, ewe mwanamke, yeyote niliyemwita. Hiyo ni kweli, sivyo? Nenda upo-. . . Kama ulivyoamini, na iwe hivyo.

Sijawahi kumwona huyo mwanamke maishani mwangu, ninainua mikono yangu, sijawahi kumwona. Unaamini Yeye yupo hapa? Alifanya nini? Aligusa kitu Fulani.

Nitageuza mgongo wangu. Mwasema, "Unawaangalia, saikolojia."

Sikilizeni, aminini. Bwana Mungu na ajionyeshe Mwenyewe Mungu.

240 Sasa ninamwona mwanamume amesimama mbele yangu. Ninazungumza tu, na, yeyote yule. Huyo mwanamume anaugua ugonjwa wa moyo. Amevaa suti nyeusi, na namna fulani ya tai ndogo ya kanali. Yeye ni mtu mfupi. Je, amesimama kwa miguu yake bado? Jina lake ni Cotes. Amini kwa moyo wako wote, na upokee uponyaji wako kama utaamini kwa moyo wako wote. Mungu akubariki, nenda nyumbani, uponywe.

Unaamini? Ninainua mkono wangu, sijawahi kumwona maishani mwangu.

Mnaamini? Basi wekeaneni mikono. “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.”

> Itakuwa Nuru wakati wa jioni,
> Njia ya Utukufuni hakika mtaipata.

241 Mnaamini hilo? Sasa, ombeaneni. Wekeni mikono yenu. . . Ombeaneni, nanyi mnaweza kuponywa, hata haitawabidi kuwa na mstari wa maombi kesho usiku.

242 Muhuri wa Mungu ni ubatizo wa Roho Mtakatifu, alama ya mnyama ni kuikataa. Mpokeeni Roho Mtakatifu!

243 Ni wangapi wanaotaka ubatizo wa Roho Mtakatifu? Simameni kwa miguu yenu. Ni wangapi wanaotaka kutiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu kwa Roho Mtakatifu? Simameni kwa miguu yenu. Simameni mkampokee. Hiyo ni kweli. Huko juu kwenye roshani, msimkatae, simeni kwa miguu yenu, mpokeeni Roho Mtakatifu. Amina. Simameni, aminini.

244 Sasa, ninyi nyote mlio na Roho Mtakatifu, angalieni ni nani anayesimama pale, simameni, na muwawekee mikono yenu. Simameni, na mwawekee mikono hao wanaomtafuta Roho Mtakatifu.

245 Hebu wahudumu wanyooshe mikono yao juu *hivi*. “Wakatuma mtu wakawaleta Petro na Yohana, naye akawawekea mikono, ndipo Roho Mtakatifu akawajilia.”

246 Bwana Yesu, ninaikabidhi ibada hii Kwako. Wajaze na Roho Mtakatifu, Bwana. Waponye, katika Jina la Yesu Kristo. Haya basi.

61-0217 Alama Ya Mnyama Na Muhuri Wa Mungu #2
First Assembly Of God Of Long Beach
Long Beach, California Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org